# CHUO KIKUU CHA NAIROBI

**MWONOULIMWENGU WA WASWAHILI**

**JINSI UNAVYOJITOKEZA KATIKA NGANO**

**NA**

**[NYONJE, JACKTONE WINSTONE**

**TASNIFU YA UZAMILI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

|MI1J1VK>3 VMVOIbdV 1SV3
hcXmn io AiisaaAiNn TA mcmG*»a1
JU-o ^ ^ ^ A R V

**2006**

University of NAIROBI Library
0472391 2

# UNGAMO

Tasnifu hii ni yangu mwenyewe na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

*"Mil- j»*

**I**

NYONJE, JACKTONE WINSTONE

(Mtnhiniw a)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu nikiwa msimamizi \va kazi hii wa Chuo Kikuu

DKT. RAYYA TIMAMMY

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yangu nikiwa msimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu

DKT. EVANS M.MBUTIA

# TABARUKU

Ningependa kutabaruku na Mke Wangu mpendwa Dorothy A. Odenyo na watoto wapendwa; Ron, Shelly, Awinja na Jeff kwa kunipa moyo wakati huu wote nimekuwa nimezamia kazi hii.

# SHUKRANI

Naungama kazi hii haingewezekana bila ya  uvumilivu, sulubu, na utafiti ulioambatana na ushauri mzomzo. Yumkini haingefikia kiwango hiki bila ya msaada kutoka mahali pengi. Kwanza ningependa sana kumshukuru mwenyezi mungu kwa kunijalia maisha, afya na mwongozo ulioniwezesha kufika daraja hii. Aidha ningependa kuwashukuru sana walimu na wasimamizi wangu kwa kujitolea kwao, ushauri mzuri walionipa. Hawa ni Dkt. Rayya Timammy na Dkt. Evans M. Mbuthia. Sitawasahau maishani mwangu.

Shukrani pia ziwaendee walimu wangu; Profesa Mohamed H. Abdulaziz, Dkt. Mwenda Mbatia, Dt. Kineene wa Mutiso, Dkt. Tom Olali, Dkt. John Habwe,Dkt. Zaja  Omboga, Bw. Ayubu' Mukhwana, Bw. B. Mungania , Dkt. Alfred  Buregeya, Bw. Hezron Mogambi. Ahsanteni  kwa kunifundisha na kuniongoza vizuri.

Aidha ningependa kuwashukuru sana marafiki zangu Dkt. Hannington Odame, Norbert Abachi, Mark Chetambe na Julius Mungai kwa mijadala ya kiusomi tuliokuwa nayo.



r

Shukrani vilevile ziwaendee wanafunzi wangu wote niliowafundisha kwa kunihimiza kubobea zaidi. Ningependa hasa kuwataja Dennis J. Odallo, wa Chuo kikuu cha Missouri, Marekani na Sammy Wandabwa wa Chuo Kikuu cha Birmingham, Uingereza kwa mijadala yao ya kiusomi..

Aidha nachukua fursa hii kuwashukuru wanafunzi wenzangu wa uzamili: Samuel Ng'ang'a rafiki mwendani na msomi; Bi. Elizabeth Katola na Bi. Esther Muli. Hongera kwa usuhuba na ushirikiano wenu.

Shukrani pia zimwendee Sheikh Ahmad Nabhany kwa ushauri na majadiliano tulioukuwa nayo Mjini Mombasa tarehe 09.04.06. Namkumbuka ndugu yangu Raphael Ondeko na mkewe Emily kwa msaada na himizo, Mungu awabariki sana.

Mwisho kabisa ningependa kumshukuru sana inke wangu, Dorothy A. Odenyo kwa uvumilivu, upweke na kazi ngumu ya kuwalea watoto wetu: Ron, Shelly, Awinja na Jeff. Mungu awabariki sana.

## MUHTASARI WA SOMO

Tasnifu hii lmegawika katika faslu nne. Sura ya kwanza inahusu pendekezo la utafiti, sababu za kuchagua somo hili, msingi wa nadharia, malengo, yaliyoandikwa kuhusu mada, upeo, haipothesia na njia za utafiti. Sura ya pili imeangazia historia ya Waswahili, ufafanuzi wa dhana ya mwonoulimwengu, elementi za mwonoulimwengu, njia za kuelezea mwonoulimwengu wa waswahili. Sura ya tatu inaangalia mwonoulimwengu wa Waswahili katika kazi ya Carl Velten: **Desturi za Waswahili** iliyohaririwa na Lydon Harries, Seira hii imeangia: Hatua mbalimbali za maisha - kuzaliwa kwa mtoto, malezi ya watoto, elimu, tohara, na ndoa. Sura ya nne ni hitimisho la tasnfiu.

UNGAMO ....... i
TABARUKU ....... ii
SHUKRANI ....... "i
MUHTASARI WA SOMO ....... iv

**SURA YA KWANZA**

1.0 Utangulizi ....... 1
1.1 Swala la utafiti ....... 3
1.2 Malengo ya utafiti ....... 4
1.3 Nadhariatete ....... 4
1.4 Upeo wa tasnifu ....... 5
1.5 Yaliyoandikwa kuhusu mada ....... 5
1.6 Msingi wa nadharia ....... 8
7. Njia za utafiti ....... 10

**SURA YA PILI**

HISTORIA NA MWONOULIMWENGU WA WASWAHILI

2.0 Utangulizi ....... 11
2.1 Historia fupi ya Waswahili ....... 11
2.2 Utawala wa Wareno ....... 13
2.3 Utamaduni wa Waswahili ....... 14
2.4 Uswahili na Uislamu ....... 15

2.5 Athari za utamaduni wa kimapokeo wa kibantu .......... 15

2.6 Athari za Uislamu .......... 16

2 7 Uamilifu na elementi za Mwonoulimwengu .......... 18

2.8 Elementi na njia za kueleza mwonoulimwengu .......... 18

2.9 Kategoria za Kifasihi .......... 19

2.10 Sanaa zisizo za Kifasihi .......... 19

2.11 Kazi Mbalimbali .......... 19

2.12 Vifaa na mavazi .......... 20

2.13 Imani na maabdi .......... 20

2.14 Mwonoulimwengu Wa Waswahili .......... 20

2.15 Mfumo wa Kiuchum .......... 21

2.16 Uwindaji .......... 21

2.17 Matumizi ya miti .......... 22

2.18 Uvuvi .......... 22

2.19 Kilimo .......... 23

2.20 Biashara na ufiigaj i .......... 24

2.21 Usafiri na usanii .......... 25

2.22 Mfumo wa kijamii .......... 27

2.23 Familia .......... 28

2.24 Koona Kabila .......... 29

2.25 Dini, itikadi na uchawi .......... 30

2.26 Namna Waswahil wanavyoelezea Mwonoulimwengu wao .......... 32

2.27 Hitimisho .......... 36

**SURA YATATU**

**UHAKIKI WA DESTURI ZA K1SWAHILI**


3.0 37

3.1 Ukusanyaji na uhariri wa Desturi za Waswahili 37

3.2 Hatua mbalimbali za maisha jinsi inavyojitokeza katika desturi za Waswahili...39

3.3 41

3.4 Ada ya akika 41

3.5 mtoto kutolewa nje 47

3.6 Wosia 47

3.7 Kunyolewa kwa mtoto 50

3.8 Mtoto kupewa jina 51

3.9 Mtoto kuota meno 52

3.10 Malezi ya mtoto 53

3.11 Ndishe na afya 53

3.12 Kinga na ulinzi wa watoto 53

3.13 Malezi ya watoto wenye mikosi 54

3.14 Elimu ya watoto 55

3.15 Elimu ya chuoni au Kiislamu 56

3.16 Elimu nje ya Chuo 58

3.17 Tohara 60

3.18 Tohara ya mtoto wa kiume 61

3.19 Tohara ya mtoto wa kike 65

3.20 Ndoa 67

3.21 Uchumba ... 68

3.22 Kikombe cha kahawa ... 70

3.23 Kupiga pamba na harusi ... 70

3.24 Elementi za mwonoulimwengu katika desturi za Waswahili ... 71

3.25 Kinga dhidi ya hatari ... 72

3.26 Nguvu ya sala ... 72

3.27 Usambazaji na uhifadhi wa maarifa ... 73

3.28 Afyabora ... 74

3.29 Ushujaa na uvumilivu ... 74

3.30 Ujamaa na mshikamano wa jamii ... 74

3.31 Ujumi na utakaso ... 75

3.32 Uyakinifu wa mwonoulimwengu wa Waswahili ... 76

3.33 Hitimisho ... 76

SURA YA NNE

4.0 Hitimisho ... 77

Marejeleo ... 82

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

**Mwonoulimwengu** ni ufafanuzi au maelezo ya kimantiki kuhusu mpangilio **wa** mambo katika **jamii na unavyoathiri** maisha ya watu na mazingira yao. Ni ile picha au taswira tunayoipata jinsi **inavyoelezewa** na mfumo **wa** dhana zinazoelezea midundo ya kimaumbile na kijamii na nafasi au **mahali** pa binadamu na jamii katika mtandao huo changamano.

Kila jamii ina namna yake ya kutazama ulimwengu wake. Ni muhali kwa binadamu kutokuwa na maoni na maono fulani kuhusu maisha na ulimwengu. Haya mawazo ya mtu binafsi hatimaye husambazwa kwa watu wengine. Mawazo mapya huchipuka na kuchukua mahali pa yaliyotangulia au mawazo ya kale huimarishwa na kuwa bora zaidi. Muda si muda mawazo haya hujikusanya katika mfumo wa mawazo ya jamii fulani. Huu mfumo wa mawazo hutupa picha au taswira ya jumla kuihusu hiyo jamii. Mfumo wa mawazo huhifadhiwa na kusambazwa kwa njia maalumu.

Vansina (1985:124) anasema kuwa habari zote katika jamii ni sehemu ya utamaduni ambayo zinadhihirika kupitia kwa taratibu za kufikiri na kutoa habari.

Mambo kadhaa muhimu yanajitokeza katika maelezo haya; mosi, utamaduni hautokani na ombwe tupu bali unatokana na kundi fulani la watu. Pili, utamaduni hubeba habari na ujumbe kuwahusu watu. Tatu, lugha ni chombo muhimu cha kutangaza utamaduni na nne, utamaduni hubeba mifumo sahili na changamano ya fikira za watu fulani na shughuli zao zote za maisha.

Kwa hivyo ni muhali kung'amua mwonoulimwengu wa watu fulani bila ya kuuelewa barabara utamaduni wao.

Kwa hivyo tunaweza kusema ya kwamba ikiwa kuna watu, sharti watu nao wanaishi katika eneo maalum la kijiografia na watu hawa wana namna yao kufasiri na kuyasukasuka mazingira kwa **mujibu** wa mahitaji yao. Mwelekeo na mtazamo wa watu hawa ni wa pamoja licha ya tofauti ndogondogo zinazozuka baina ya watu binafsi. Kimsingi mtazamo na mwelekeo wao ni mmoja kuhusu ulimwengu.

Kwa mujibu wa maelezo ya wataalamu kama vile Lewis (2002), Noor Shariff (1988), na Shihabuddin Chiraghdin (1977), na tunaona ya kwamba utamaduni ni tukio la kiakili. Yaani maana na fasiri mbalimbali hutokana na uwezo wa akili za watu kufikiria. Fasiri na maana lazima zikubaliwe na watu wote wa kundi hilo. Kwa hivyo tunaweza kuhitimisha ya kwamba kila kundi lolote la watu lililo na utamaduni lina uwezo wa kutimia akili zao barabara kubuni na kavumbua. Mchakato mzima wa fikira ndiyo huibua 'mawazo' yanayotumiwa kuyasukasuka mazingira na kuyabadili. Hali hii imedhihirika katika vifaa, asasi na taasisi mbalimbali za utamaduni huo. Ikiwa ni hivyo waswahili wamebuni, wamefikiria na kuvumbua. Lugha yao imedhihirisha sifa hizi.

Tamaduni zote huwakilisha na kuwasilisha mwonoulimwengu fulani kama walivyosema Vansina( 1985:24) na Lewis(2002). Huwezi kufasiri barabara mwonoulimwengu wa watu fulani ikiwa hujauelewa utamaduni wao. Kila kundi la watu huulinda na kuusambaza utamaduni kwa njia mbalimbali kwa kutumia ngano, nyimbo, mashairi, sanaa ya uchoraji, na matambiko. Overholt na Callicott (2002: 197) wanasema ya kwamba watu mbalimbali hawayapangi mawazo na fikira zinazotokana na tajiriba zao za maisha kwa namna moja kwa sababu ya mionoulimwengu tofauti tofauti inaoyowakilishwa na tamaduni mbalimbali

Tasnifu hii itaangazia namna desturi za waswahili zilivyo na dhima kubwa ya kuelezea mwonoulimwengu wao.

## 1.1 Swala La Utafiti

Mada ya tansifu hii ni **Mwonoulimwengu wa Waswahili Jinsi Unavyojitokeza katika Desturi za Waswahili** Kazi hii inajishughulisha na namna Waswahili wanavyofasiri ulimwengu wao kwa mujibu wa asasi mbalimbali zinazojitokeza katika desturi zao. Asasi hizi ni kama vile **ndoa na** arusi, kuzaliwa kwa watoto, tohara, elimu, kazi zao na ufasiri wao wa ujumi. Aidha kazi hii itazitathmin sherehe zinazoambatana na asasi hizo, mkazo ukitiliwa kwenye uamilifu na dhima yake katika jamii hii.

Tunasisitiza ya kuwa utamaduni unahusishwa na watu fulani katika mazingira fulani. Utamaduni huangazia mfumo mzima wa imani, fikira, mitazamo, ujumi, hisia na shughuli zote za watu hao. Kila utamaduni una ishara na misimbo mbalimbali ya kuhifadhi na kusambaza ujumbe huo wa kitamaduni. Ni wale tu walio na tajiriba na ufahamu mkubwa wa utamaduni wanaweza kuzisimbua ishara na misimbo hiyo. Msimbo mkuu ambamo ndani yake kuna misimbo mingine ni lugha. Kuifahamu lugha ya watu ni kuwafahamu watu hao. Siyo tu ule uwezo wa kuweza kuisoma na kuiandika ya lugha hiyo bali ni kusikiliza, kuizungumza, kuihisi, kushiriki na kujihusisha nayo, kuifikiri na hata kuionja. Lugha ni mkondo huo kuwa mkubwa zaidi. Lugha ni muumano wa misimbo. Ni mchakato changamano wa misimbo na hatua mbalimbali za maisha. Misimbo hii ni kama vile ngano, mashairi, nyimbo, visasili, hurafa, misemo na mafumbo.

Licha ya kuwepo kwa mikusanyiko mighi ya ngano na kazi zingine za kifasihi zilizofanywa kwa kiasi kikubwa na wamishenari, wasafiri, na watawala wa kikoloni, mingi ya mikusanyiko hiyo

**haijafanyiwa uhakiki** hasa ule unaolenga kuonyesha mwonoulimwengu wa waswahili. Tasnifu hii **inahakiki** mkusanyiko wa Carl Velten: **Desturi za Waswahili** uliyohaririwa na Lyndon Harries. **Uhakiki** wetu utazitathmini asasi mbalimbali zinazojitokeza katika hatua mbalimbali za maisha na namna asasi hizo zinavyoelezea mwonoulimwengu wa waswahili. Kazi hii imechaguliwa kwa **sababu** inaelezea desturi za mmojawapo ya makundi ya waswahili.

## 1.2 Malengo Ya Utafiti

Tasnifu hii ina malengo yafuatayo: -

(i) Lengo kuu la tasnifu hii ni kuelezea mwonoulimwengu wa Waswahili.

(ii) Kuzitambua elementi mbalimbali za mwonoulimwengu wa Waswahili.

(iii) Kujadili namna utamaduni wa Waswahili unavyoelezea maono, mahitaji na matarajio yao kupitia desturi zao.

(iv) Kazi hii itazitathmini asasi mbalimbali zinazojitokeza katika **Desturi Za Waswahili** na namna zinavyoelezea mwonoulimwengu na waswahili.

(v) Kazi hii itachambua na itathmini sherehe zinazoambatana na hatua mbalimbali za maisha **kama** vile - kuzaliwa, kulelewa, kuoa. Jinsi zinavyojitoeza katika **Desturi Za Waswahili.**

## 1.3 Nadharia Tete

**Tasnifu hii** ina nadharia tete zifuatazo: -

(i) Waswahili wana mwonoulimwengu wao.

**(ii)** Mwonoulimwengu wa Waswahili huelezewa katika desturi zao.

**(iii)** Maisha ya Waswahili hupitia hatua mbalimbali: kuzaliwa, kuoa na kufa.

(iv) Waswahili wana asasi mbalimbali zinazoyaongoza maisha yao.

(V) Kila hatua ya maisha ya Waswahili huambatana na sherehe maalumu.

## 1.4 Upeo Wa Tasnifu

**Tasnifu hii** itajikita tu upande wa hadithi zilizokusanywa na Carl Velten, zikahaririwa na Lyndon Harries **(1964).** Mkusanyiko huu umegawika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza **ni Desturi za Waswahili** na sehemu ya pili ni **Safari za Waswahili** Tasnifu hii itashughulikia sehemu ya **kwanza: Desturi za Waswahili.** Tasnifu hii itachambua hatua mbalimbali za maisha anazopitia **mwanadamu** tokea kuzaliwa kwake hadi hatua ya ndoa. Waswahili wanaorejelewa ni Wamrima wanaopatikana katika eneo la Tanga, Kusini mwa pwani ya **Afrika** Mashariki. **Kipindi kinachozungumziwa** ni cha mwaka wa 1890.

## 1.5 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo

Wataalmau wafiiatao katika kazi zao mbalimbali wameigusia mada ya tasnifu. Njogu na Chimerah (1999), Abdulaziz,M( 1995,1979), Noor Sharrif(1988), J. D. Rollins (1983), Rajmund Ohly (1981), Ian Knappert (1979), Finnegan (1970), Ruth Finnegan (1970), M. S. Farsy (1960), Prins (1967). J. S. Mbiti (1966),

Njogu na Chimerah (1999) wanafafanua tu kipera cha ngano kwa kuzirejelea sifa, za utanzu huu na namna unavyoweza kufundishwa.Kazi hii imegusia mambo machache kuhusu mwonoulimwengu wa Waswahili.

Abdulaziz (1995,1979). Katika kazi zake amezungumzia kuhusu historia ya Kiswahili. **Amezirejelea** athari za Uislamu, kuathiriana baina ya Waswahili na makundi mengine ya watu. **Anaeiezea** kuhusu mwonoulimwengu wa Waswahili lakini kazi zake hasa ile ya (1979), anajikita **sana** katika ushairi.

Rollins (1983), vilevile anaainisha tanzu mbalimbali za nathari ya Kiswahili. Miongoni mwa kazi zilizorejelewa ni mikusanyiko ya Carl Velten. Mtaalamu huyu anatambua umuhimu wa kazi ya Velten ya **Desturi Za Waswahili** anapoisifia kuwa ni ya kiwango cha juu na muhimu katika kuelewa utumaduni na mwonoulimwengu wa Waswahili. Hata hivyo kazi hii imegusiwa tu bila kuhakikiwa.

Ohly (1981), katika kazi yake ameshughulikia nathari ya Kiswahili. Katika kuainisha utanzu **ameibuka** na kategoria saba za nathari ya Kiswahili. Miongoni mwa kategoria hizo ni kazi za Carl Velten ambazo ameziweka katika kategoria hizi:

(i) Nathari za kiethnografia - Kazi ya Velten iliyoainishwa hapa ni: **Desturi za Wasuaheli** vilevile ameitaja kazi ya M. S. Farsy: **Kurwa na Doto** ambayo tayari imerejelewa katika tasnifu hii.

(ii) Nathari za safari - mkusanyiko wa Carl Velten - **Safari za Wasuaheli.** Tasnifu hii inahakiki kazi ya kwanza yaani **Desturi za Wasuaheli.** Ohly ametaja tu kazi hii bila ya uhakiki wowote.

Knappert (1979), katika kazi yake ya **Myths and Legends of the Swahili;** amekusanya visasili, visakale na hadithi za waswahili. Kazi yake ni muhimu kwa sababu imetambua kuwepo kwa jamii ngano **ya** waswahili walio na utamaduni wao ambao huelezewa na kuhifadhiwa katika visasili, visakale na. Mtaalamu huyu katika dibaji ya kazi yake amegusia elementi muhimu za mwonoulimwengu wa Waswahili. Aidha amegusia athari za Uislamu katika utamaduni wa Kiswahili. Kazi yetu imejikita upande wa mkusanyiko wa Carl Velten.

Prins (1967), anazungumzia kuhusu maisha ya Waswahili kwa jumla. Amezungumzia kuhusu desturi zao, kazi zao, mpangilio na utaratibu wa mambo katika jamii hii, mazingira yao, hali ya hewa Kazi hii ni muhimu katika kutusaidia kuelewa maisha na desturi ya waswahili kwa sababu inatambua kuwepo kwa waswahili walio na utamaduni wao. Hata hivyo kazi hii haingilii kwa undani vipera vya kifasihi na jinsi vipera hivyo vinvyotumiwa kuhifadhi na kusambaza utamaduni.

Finneuan (1970) katika kazi yake ameshughulikia fasihi simulizi ya kiafrika. Ameanzia kwenye nadharia hadi kwenye tanzu mbalimbali za fasihi simulizi miongoni mwa kazi za kinathari alizotambua ni hii ya Carl Velten: **Desturi Za Waswahili.** Hata hivyo licha ya kazi nzuri aliyoifanya, mtaalamu huyu alishughulikia eneo pana zaidi la fasihi simulizi jambo lililomfanya kutaja baadhi ya kazi muhimu za fasihi simulizi kama alivyofanya hii ya Velten.

Mbiti (1966) katika mkusanyiko wa hadithi za Kikamba aliouhariri, anatambua athari za utamaduni wa Kiswahili kwa hadithi hizi za Kikamba. Kazi hii i ya Mbiti ni muhimu kwa njia mbili; kwanza inatambua umuhimu wa ngano kama nyenzo muhimu ya kusambazia na kuhifadhia utamaduni wa jamii fulani. Jambo ambalo litashughulikiwa katika kazi hii. Pili anatambua kuwepo kwa utamaduni wa Kiswahili na athari za utamaduni huo kwa makundi yaliyotangamana na Waswahili.

Farsy (1960) amesimulia hadithi ya mapacha wasichana yaani Kurwa na Doto. Mtaalamu huyu anasimulia maisha yao yote kwa kuungazia hatua mbalimbali za maisha waliopitia - kuzaliwa, malezi, elimu, ndoa, mahusiano yao, kuchumbiana, kifo. Aidha mwandishi amesimulia kwa ufasaha, sherehe na itikadi zilizoambatana na kila hatua. Kazi hii kwa hakika imemulikia desturi za waswahili. Na Waswahili wanaozungumziwa ni wa Unguja. Kazi hii ni muhimu kwa sababu

inaelezea kuhusu falsfa na mwonoulimwengu wa waswahili. Tasnifu hii haisimulii bali inahakiki desturi itikadi na falsafa ya Waswahili ikilenga kuweka bayana mwonoulimwengu wa Waswahili. Pili tasnifu hii inwaangazia Waswahili wa Mrima.

## 1.6 Msingi Wa Nadharia

Tasnifu hii inadhamiria kutumia nadharia za Uamilifu na Unegritudi katika kuhakikia mada yetu. Nadharia ya uamilifu imehusishwa sana na wanadharia Malinowski, Evans Pritchard na Radcliffe Brown Nadharia hii inaangali fasihi simulizi kwa mujibu wa dhima yake katika jamii. Nadharia hii hutuelekeza kuelewa umuhimu wa fani za fasihi simulizi katika jamii. Nadharia ya uamilifu huona utamaduni wa binadamu kwa mujibu wa uhusiano wa vipengele ambavyo vinasaidia kuelewa muundo wa jamii. Vipengele hivi vya utamaduni huwa na uamilifu mbalimbali katika jamii. Msingi wa jamii yeyote ni uamilifu wa vipengee hivi pamoja na asasi mbalimbali zinazothaminiwa na jamii.

Udhaifu mkubwa wa nadharia hii ni kule kusisitiza uamilifu na utendaji wa fasihi simulizi na wala siyo ujumi wake. Kulingana na Finnegan (1970) nadharia hii inchukulia fasihi simulizi kama si kinachojismamia kama taaluma. Isitoshe, nadharia husisitiza ukale wa malighafi ya fasihi simulizi na katika kufanya hivyo hupuuza mionoulimwengu ya jamii mbalimbali jinsi inavyojitokeza katika vitanzu mbalimbali vya fasihi simulizi. Si ajabu mikusanyiko mingi ya hadithi iliyokusanywa na wamishenari na wasomi wengine wa kimagharibi ama haikuchanganuliwa au iliainishwa katika misingi ya uamilifu wake katika jamii. Mathalani ngano za maadili, ngano za wanyama, ngano za miungu . Nadharia ya uamilifu itatumiwa katika tasnifu hii kujadili uamilifu wa asasi mbalimbali zinazojitokeza katika desturi za waswahili, uamilifu wa elementi za mwoulimwengu wa waswahili.

**Kwa sababu** ya mapengo yanayojitokeza katika nadharia ya uamilifu, tasnifu **hii** itatumia nadharia ya **pili** Nadharia yenyewe ni nadharia ya unegritedi. Nadharia hii ilichumbuka kutokana na mawazo ya **wasomi** wa asili ya kiafrika - kutoka ndani na nje ya Afrika - waliowahi kuwa chini ya utawala **wa** Kifaransa Athari za mfumo wa kikoloni ziliwafanya wasomi hawa kuanza kujisaka katika nafsi zao **waking'**ang'ania utambulish zaidi kama watu weusi. Miongoni mwa waasisi wa Unegritudi **walikuwa:** Aime Cesaire kutoka kisiwa cha Martinique, Leopold Senghor kutoka Senegal na Leon **Damas kutoka** Guyana.

Unegritudi unasisitiza umuhimu wa kuutuza na kuusifu utamaduni wa mtu mweusi pamoja na kuionea fahari fasihi mweusi kwa njia inayoangazia matatizo yanayomkabili, unegritudi kimsingi, ulikuwa kama kichocheo kwa mtu mweusi kuitumia kale kama kifaa cha kuupinga mkondo wa kisaikologia unaotokana na falsafa kengeushi ya usilimisho. Ni katika manzili haya ambapo waasisi wa unegritudi walizuka na mikondo ya kimawazo inayosisitiza umbuji Wamitila (2002). Dhamira kuu za unegritudi zilikuwa: -

(i) Suala la ujitambuzi wa Mwafrika.

(ii) Mjadala kuhusu mtindo wa kitaduni wa maisha ya Waafrika.

**(iii)** Shutuma dhidiya ukoloni wa ugwaji mkono wa ukoloni huo.

(iv) Vita dhidi ya ukoloni Mamboleo na hali ya wasomi wa kiafrika leo.

Nadharia hii inawafiki kazi yetu kwa sababu inasisitiza hadhi ya utamaduni wa mtu mweusi pamoja na njia zake mbalimbali za kuusambaza. Nadharia hii inatambua kuwepo kwa mionoulimwengu mbalimbali.

**Tutazitumia** hizi nadharia mbili kuhakikia kazi hii kwa sababu, mbali na kujishughulisha na ujumi **na ufundi** uliotumiwa kuwasilisha mawazo mbalimbali, lengo la kazi hii ni kutathmini uamilifu wa **desturi za Waswahili** kama nyenzo ya kusambaza na kuhifadhia utamaduni. Aidha tutaangalia **uamilifu** wa asasi mbalimbali zinazojitokeza katika **Desturi Za Waswahili.**

## 17 NjiaZa Utafiti

Tasnifu hii imetumai ushahidi kutoka kazi zingine zinazohusiana na mada ya tasnifu. Aidha tasnifu imetegemea mazungumzo ya wataalamu, niliozungumza nao. Mtaalamu niliemtegemea sana alikuwa; Sheikh Ahmad Nabhany, niliyepata fiirsa ya kuzungumza naye tarehe 09.04.06. Kuanzia **saa** tatu **za** asubuhi, Fort Jesus, Mjini Mombasa. Mtaalamu huyu aliungama ya kwamba Waswahili walikuwa na wangali na desturi zao. Kulingana na Nabhany, desturi hizi zingalipo ingawa zingine zimeanza kupotea kwa sababu za athari za elimu ya kisasa na dini za Ukristo na Uislamu. Sheikh Nabhany anakubali kuwa utamaduni wa Kiswahili umeathiriwa na Uislamu, na utamaduni kutoka makundi mengine ya kigeni, kibantu na kikushiti.

ft

# SURA YA PILI

# HISTORIA NA MWONOULIMWENGU WA WASWAHILI

## 2.0 Utangulizi

Waswahili kama jamii zingine wana historia yao na mwonoulimwengu wao unaowatambulisha kama jamii miongoni mwa jamii zingine. Sura hii itajishughulisha na mambo yafuatayo: Historia fupi ya Waswahili, kuzuka kwa utamaduni wa Waswahili, ufafanuzi wa dhana ya mwonoulimwengu, mwonoulimwengu wa Waswahili katika utamaduni wao, njia za kueleza mwonoulimwengu huu.

## 2.1 Historia Fupi ya Waswahili

Suala la Mswahili ni nani limezua mijadala mingi'miongoni mwa wasomi. Baadhi ya mijadala hiyo imeelezea Mswahili kuwa Chotara, Mwarabu, Mbantu au Mtu yeyote mjanja. Lakini kwa minajili ya mada ya tasnifu, nitaelezea Waswahili kuwa kundi la Wabantu wanaoishi pwani ya Afrika Mashariki kwanzia kusini mwa Mogadishu hadi sehemu za Msumbiji pamoja na visiwa vinavyopatikana katika Bahari ya Hindi yaani Zanzibar, Pemba, na Comoro. Historia fupi ya waswahili ni muhimu kwa sababu inatupa fursa ya kuona ukuaji wa utamaduni wa Waswahili, athari za makundi mengine yaliotangamana na Waswahili na namna athari hizi zilivyoathiri mwonoulimwengu wao. Aidha Historia ya Waswahili inatupa

fursa ya **kufahamu** wapi waliishi Waswahili, jinsi mazingira walimoishi yalivyothiri mwonoulimwengu wao.

Waswahili walikuwa na maingiliano ya muda mrefu na watu wa sehemu mbalimbali za dunia hata kabla ya majilio ya Uislamu. Maingiliano haya yaliwafanya Waswahili kuwa **maarufu** sana zama hizo. Maingiliano ya Waswahili na watu wa janibu zingine za duniani **yametajwa** katika kazi mbalimbali zilizoandikwa.

**Periplus of The Erythrean Sea,** kazi iliyotungwa katika karne ya kwanza **B. K.** na Mgriki mmoja ambaye jina lake halijulikani, inataja kufanyika kwa biashara baina ya wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki na wachuuzi wa Kiarabu. Isitoshe kazi hiyo inataja kuwepo kwa miji mistawi katika pwani hiyo iliyofanya biashara na Wahindi, Waarabu na wamisiri. Bidhaa za biashara zilikuwa nyingi. Miongoni mwazo zilikuwa: nguo, nafaka, sukari, mafiita ya kupikia, vito mbalimbali kama vile fedha, shaba, vipusa. Aidha kazi hii inataja kuwepo kwa mitego ya samaki, mashua na mitepe.

Kufikia katikati mwa karne ya pili, pwani ya Afrika Mashariki ilikuwa imestawi katika biashara ya kimataifa na kuhusisha mataifa kama vile Urumi. Ni kutokana na maingiliano haya ndipo Warumi walipita pwani ya Afrika Mashariki yaani Azania. Biashara hii ilistawisha miji ya pwani iliyokuwa ikitumiwa kama vituo vya biashara.

AJ-Masud (945 B.K) katika kitabu chake **Murujal Dhahab** anataja watu wa Qumbalu (inakisiwa kuwa labda Pemba) ambao walihusisha Waislamu na wapagani. Watu hawa

alizungumza lugha iliyojulikana kama Kizanji (lugha hii inakisiwa kuwa aina fulani ya Kiswahili).

Mwanahistoria Neville Chittick akinukuliwa na Noor Shariff (1988: 2-3) anatuelezea kuwa, ijapokuwa utajiri wa miji ya Waswahili ulitokana na biashara yao na nchi zilizoko katika Bahari ya Hindi, ilibidi kwanza wapate mali kutoka bara iii kuweza kufanya biashara hiyo. Waswahili walinunua mali kama vile pembe za ndovu na vipusa na kuvitumia vitu hivyo katika kununulia au kubadilishana na mali kama vile vyombo vya fedha na dhahabu, vitambaa vya hariri, manukato na bizari kutokana na wakaazi wengineo waishio katika nchi za pwani ya Bahari ya Hindi na hata tangawizi kutoka Uchina.

Rhandall L. Powels akinukuliwa na Mohamed Abdulaziz (1955: 142-156) anaelezea kuhusu awamu tatu za maendeleo ya wakazi wa pwani. Awamu ya kwanza (baina ya miaka 800-1100 B.K) ilihusisha makundi ya Kisabaki, Kibantu na Wasomali wa kale. Awamu ya pili (1100-1300 B.K) kuzuka kwa miji kama vile Shanga, Manda, Pate, Unguja, Ngazija na Kilwa. Awamu ya tatu ilikuwa- upeo wa historia ya pwani, ustaarabu na ustawi wake kiuchumi.

## 2.2 Utawala wa Wareno

Wareno walivamia na kutawala pwani ya Afrika Mashariki baina ya miaka ya 1505 hadi 1698 B.K. Utawala wao ulikuwa wa kikatili uliohusisha uporaji na uharibifu mkubwa sana wa miji mistawi ya pwani ya Afrika Mashariki. Juhudi za wenyeji wa pwani kupambana na vikosi vya Kireno vilivyotumia silaha bora ikilinganishwa na zao duni, hazikufua dafu.

Shariff Noor (1988: 4) akiwanukuu wanahistoria Coupland na Basil Davidson anatuelezea **kuwa** miji kama vile Mombasa na Faza ilihujumiwa vikali zaidi. Wareno hawakuteka nyara tu bali waliuwa kila chenye uhai walichokiona, wanaume, wanawake, watoto, hata mbwa **waliofugwa** majumbani pamoja na makasuku pia vidau, mashua na ngarawa zilizokuwa **bandarini** zilichomwa moto. Mashamba yote yaliharibiwa. Milima ya ngawira ilikusanywa - dhahabu, fedha, pembe za ndovu, ambari, ng'ombe, na vyakula vingine. Ngawira ilikuwa kubwa mno, hata ikabidi mali nyingine iachwe, kwani hakukuwa na nafasi katika meli zao.

Licha ya ukatili wao Wareno waliathiri,utamaduni wa Waswahili. Athari zilikuwa majina ya vitu kama vile; karata na matunda - Nanasi, samaki - kamba, vifaa - meza, na gwaride. Majina haya ni sehemu ya msamiati wa Kiswahili.

## 2.3 Utamaduni wa Waswahili

Maingiliano baina ya wakazi wa pwani ya Afrika Mashariki na wale wa sehemu zingine za dunia hasa wa Mashariki ya Kati na ya Mbali ulikuwa'na athari kubwa sana katika utamaduni wa Waswahili. Wageni wengi kutoka Asia waliokuja pwani kwa shughuli za biashara, walivutiwa sana na takrima za wenyeji pamoja na utamaduni hata wakaamua kuhamia pwani. Mbali na kuhamia huku wageni hawa walioana na wenyeji hata wakafikia kiwango cha kuwacha utamaduni wao na lugha hata wakawa wanajiita Waswahili. Kuna nasaba nyingi za kiarabu zilizoguria pwani ya Afrika ambako zinaishi hadi leo lakini zinajinasibisha zaidi na Uswahili kuliko Uarabu.

**Kilele** cha mahusiano haya kilikuwa wakati wa utawala wa Sultan Seyyid Said ambaye alivutiwa na bandari na hali ya hewa ya pwani hadi akahamisha makao yake kutoka Maskati Oman hadi Zanzibar. Seyyid Said aliwakaribisha Waarabu na Wahindi katika pwani ili wamsaidie kuudhiti ufanisi wake wa kisiasa na kiuchumi. Ilikuwa wakati huu utamaduni wa Kiswahili ulipoathiriwa sana na tamaduni zingine hasa Uarabu. Mitindo ya ujenzi, mapishi na takribani kila kitu kilibadilika. Utamaduni wa Kiswahili uliimarishwa sana kutokana na athari hizi. Lugha ya Kiswahili ikawa ndiyo lugha ya mawasiliano baina ya Waafrika, Waarabu na Wahindi. Waarabu na Wahindi walichukua Kiswahili kama lugha yao hata wakawa wanaitumia majumbani mwao Abdulaziz,1995. Kiswahili kilikopa maneno mengi kutoka kwa Kiarabu. Ni muhimu hapa kutajwa kuwa, licha ya Waarabu kusimilishwa katika utamaduni wa Kiswahili, hawakupoteza kabisa utambulisho wao.

### 2.4 Uswahili na Uislamu

Ni muhali kuzungumzia kuhusu utamaduni wa Kiswahili bila ya kurejelea athari za Uislamu. Wakazi wa pwani ya Afrika Mashariki, waliipokea na kuikumbatia dini ya Kiislamu. Uislamu ambao ulisambazwa katika Kiarabu uliacha athari kubwa sana katika utamaduni wa Kiswahili. Kwa hivyo tunapozungumzia kuhusu utamaduni wa Kiswahili, tunarejelea utamaduni mahuluti uliohusisha utamaduni wa kimapokeo wa Kibantu na Uislamu.

### 2.5 Athari za Utamaduni wa Kimapokeo wa Kibantu

Majirani wa karibu sana wa Waswahili yalikuwa makundi ya Kibantu yajulikanao kama Wamijikenda na Wapokomo. Mbali na makundi haya ya kibantu, kulikuwa na makundi ya

Kikushiti kama vile Wagalla na Waoromo. Makundi haya yalihusiana na Waswahili iashara gaacjhi ya makundi haya yamesimilishwa na utamaduni wa Kiswahili kiasi kwamba inakuwa vigumu kujua asili yao. Mfano ni kundi la Kimijikenda lijulikanalo kama Wadigo.

Maingiliano baina ya makundi haya na Waswahili yaliacha athari kwa utamaduni wa Waswahili Athari kubwa ilikuwa upande wa fasihi simulizi ambayo imekita mizizi miongoni mwa makundi haya ya Kibantu. Kwa mfano Wagalla wanatajwa sana katika ule utenzi maarufu wa Fumo Liyongo kama wahusika muhimu walioathiri maisha ya Shujaa Liyongo.

Isitoshe Waswahili wanakuwa na itikadi katika mambo ya uchawi, mizimu, kupungana pepo. Kulikuwa na pepo wa kuleta maafa na wale wa kuleta heri. Imani na itikadi hizi zilikuwa sehemu muhimu sana ya utamaduni wa kimapokeo wa Waswahili. Imani hizi zinaanza kupotea kutokana na kupigwa vita na Uislamu na hali kadhalika elimu ya kimagharibi. Fasihi ya Kiswahili inadhihirisha athari hizi. Na kwa upande wa lugha, muundo lugha wa Kiswahili kufikia sasa ni ule wa Kibantu. Kipengee muhimu ni mofolojia ya maneno yake pamoja na mpangilio wake na ngeli ambao unaoana sana na wa lugha zingine za Kibantu.

### 2-6 Athari za Uislamu

Tumeshataja kuwa maingiliano baina ya wakazi wa pwani na janibu za Mashariki ya Kati na >a Mbali zilisababisha kuathiriana pande zote. Utamaduni wa Kiswahili ulipata athari katika

vipengee vyake mbalimbali. Mathalani, sanaa ya Kiswahili imeathiriwa pakubwa na sanaa za kiarabu jinsi inavyionekana katika michoro na nakshi katika vinyago, milango, mavazi, majumba na hata katika viungo vya mwili kama vile mikono, miguuni na usoni.

Athari nyingine ni iliyohusisha mpangilio wa miji mitindo ya ujenzi, barabara na hata bustani, wakazi wa mijini walipangiliwa kulingana na matabaka mbalimbali. Kwa jumla mtindo wa maisha ingawa ulikuwa wa Kiswahili, lakini ulidhihirisha athari nyingi za mitindo ya Uislamu. Ni hali hii iliyowapelekea wageni na wasomi wengi wa kimagharibi kudai ya kwamba utamaduni wa Kiswahili una asili yake Mashariki ya Kati. Madai ya aina hii yalielekea kupuuza mchango wa Waswahili wenye asili ya Kiafrika.

Athari kubwa ya Uislamu ni falsafa ya kiislamu kuhusu maisha kwa jumla hasa mwonoulimwengu wa kila mtu katika jamii, matarajio ya kila mja na mwenendo na tabia ya kila mja katika jamii. Falsafa hii imeathiri sana fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya mambo yanayotiliwa mkazo ni kama vile kuwajali wazazi kwa mfano kuwapa heshima. Isitoshe sifa zifuatazo zinasisitizwa kuwa nzuri - kutojinaki, ujasiri, utu, ukweli na tabia nzuri kila wakati. Mbali na hayo, Uislamu ulikataza mambo yafiiatayo ambayo kila mtu muadilifu hakutarajiwa kujihusisha nayo: Ulafi, uchoyo, kiburi, wivu, usharati, ubinafsi, tamaa, ukosefu wa uaminifu na madharau kwa watu wengine. Falsafa hii ilisisitiza umuhimu wa mja kujitahidi maishani kufikia maadili haya yote. Hata hivyo ni wachache walioyatimiza yote.

## 2.7 liamilifu na Element! za Mwonoulimwengu

Uamilifi[1] mkubwa wa mwonoulimwengu ni kumsaidia binadamu kuelezea uyakinifu na halisi unaozungukia maisha yake. Hali hii humsaidia kukitegua kitendawili cha yale **niambo** au nguvu fulani ambazo haziwezi kueleweka kwa njia rahisi.

**Pili** mpangilio huu wa kimantiki wa uhalisi na uyakinifu humsaidia binadamu kutoa makisio ftilani kuhusu matukio na wakati. Na katika kufanya hivyo binadamu huyu hupata fursa ya **kuyathiti** barabara matukio hayo. Baadhi ya matukio haya muhimu ni zile hatua zake mbalimbali za maisha kama vile kuzaliwa, kubaleghe, tohara, kuoa au kuolewa na kufa. Kila moja ya hatua hizi huambatana na misukosuko mbalimbali. Na kama haidhibitwi basi itakiangamiza kizazi chake!

Kwa hivyo, utulivu, mipangilio ya mambo katika jamii, njia za ibada, sherehe zinazoambatana na tukio fulani, ari na mbinu za kuishi raha mustarehe ni mambo yanayowezekana iwapo binadamu anaelewa ulimwengu ulivyo na zile nguvu zinazosababisha hali kuwa hivyo. Ung'amuzi wake ni hatua muhimu kuelekea udhibiti.

Mwonoulimwengu ni dhihirisho la uwezo wa jamii, mahusiano, namna jamii hiyo inavyojiendeleza, upatanisho, ndoto, ulinzi, fikira, hifadhi ya mawazo ya jamii. Jamii huwa na namna mbalimbali za kueneza na kueleza mwonoulimwengu wake.

### Element! na njia za kuelezea mwonoulimwengu

j^vonoulimwengu wa unaweza kuelezewa njia mbalimbali, njia hizo zimegawika katika kategoria zifuatazo; kategoria za kifasihi, sanaa zisizo za kifasihi. Kazi mbalimbali; vifaa; majina; Imani, maadili na maabadi, viapo.

## 2 9 Kategoria za Kifasihi

Kategoria hii huhusiha visasili, visakale, hurafa, nyiimbo na densi, ngoma, mashairi.ngano, vitendawili, misemo, methali, miviga, ulumbi, riwaya, tamthilia, hadithi fupi. Vipera hivi vyote vya fasihi huibuka kutokana na utamaduni wa watu fulani. Huelezea filosofia na mwonoulimwengu wa watu hao. Ni vipera hivi vinavyodhirisha ujumi na uamilifu wa asasi mbalimbali katika jamii husika.

## 2.10 Sanaa zisizo za Kifasihi

Kategoria hii huhusisha sanaa kama vile; uchoraji, ufinyanzi, utarizi, ususi. Sanaa hizo mbali na kutuelezea kazi mbalimbali zinazofanywa na watu wa jamii husika, vilevile hutuelezea umuhimu unaowekwa kwenye ujumi. Sanaa hizi ni 'dhihirisho kwamba watu wa jamii husika, vilevile hutueleza umuhimu unaowekwa kenywe ujumi. Sanaa hizi ni dhihirisho kwamba watu wa jamii husika wana uwezo wa kufikiria na hata kuunda vitu mbalimbali. Sanaa hizi vilevile huangazia kuhusu suala la vipawa katika jamii. Yaani umuhimu wa vipawa katika jamii.

### Kazi Mbalimbali

Kazi mbalimbali kama vile uvuvi, kilimo, uhunzi, uwindanji, useremala, ufugaji na usanaji wa vyombo mbalimbali huweza vile vilevile kuelezea mwonoulimwengu wa jamii fulani.

x\ hizi huelezia Mwonoulimwengu wa jamii fulani. Kazi hizi huelezxea kuhusu mpangilio wa jamii na juhudi . Aidha kazi hudumisha mahusiano na mtagusano baina ya watu wa jamii moja au baina ya jamii mbalimbali, kazi ni nyenzo muhimu ya uzalishaji ambao unategemewa na jamii kwa uhai wake.

## 2.12 Vifaa na Mavazi

Vifaa ni muhimu kwa sababu ndivyo hutumiwa kutekelezea shughuli mbalimbali. Vifaa ni vya aina nyingi-vifaa vya burundani, ibada, kazi, kupitia kwa vifaa hivi tunaweza kufahamu shugulhi mbalimbali zinazofanywa na jamii husika. Aidha tunaweza kufahamu mambo yanayothaminiwa au yasiyothaminiwa na jamii hiyo. Mavazi vilevile mbali na kutuelezea hali ya ujumi ya jamii fulani, huweza kutelezea kuhusu filosofia ya jamii husika kwa mfano, vazi la leso miongoni mwa jamii ya Waswahili huwa na maandishi/misemo fulani ambayo huelezea falsafa ya Waswahili.

## 2.13 Imani na maabdi

Imani hutuelezea kuhusu mahusiano ya jamii na Mungu. Kupitia kwa imani, tunaweza kufahamu maadili ya jamii hiyo. Imani huifanya jamii kuwa imara.

## 2.14 Mwonoulimwengu Wa Waswahili

Waswahili wana wanaolimwengu wao uliyohusisha namna walivyoufasiri ulimwengu, mwonoulimwengu ambo kimsingi ulikuwa wa kibantu lakini uliadhiriwa sana na Uislamu. Chiraghdin akinukuliwa na Noor Shariff (1988: 8-9) anasisitiza kuwepo kwa kabila la

**jswahili waliokuwa** na ada, itikadi, mila na desturi, arusi, matanga, majando, majina, arika na magoma ambayo husheheni mawazo na maliwazo yao, tamaa zao na utu wao.

Jambo **ambalo** linasisitizwa hapa ni kwamba Waswahili kadiri walivyotangamana na **azingira** yao, waliibuka na mifumo thabiti ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mifumo ndiyo msingi wa mwonoulimwengu wao. Mifumo hii yote imezungumziwa katka **Desturi** za **Waswahili.**

## 2.15 Mfumo wa Kiuchumi

Waswahili walijishughulisha na mambo mbalimbali ya kiuchumi walioyategemea kujikimu maishani. Shughuli za kiuchumi zilikuwa: uwindaji, matumizi ya miti, uchunaji wa matunda, kilimo, ufugaji, biashara, ubaharia, usafiri, sanaa za mikono kama vile - uchimbaji na uchongaji mawe, viwanda vidogo, utarizi, usukaji, ususi, ufinyanzi, uhunzi, useremala.

## 2.16 Uwindaji

Waswahili walijushughulisha na uwindaji kama starehe au kama njia ya kulinda mimea yao. Uwindaji wa starehe hasa ulifanywa na mabwanyenye waliotumia bunduki katika shughuli **hiyo.** Uwindaji mwingine ulitumia mikuki, nyuta, mishale na mitego. Mbali na kutumia silaha hizi, mbwa walitumiwa kuwasaidia wawindaji. Baadhi ya wanyama waliowindwa waiikuwa: ndege, nyoka, ndovu, tumbili, nguruwe, swara na paa. Matumizi ya nyuta na mishale yametajwa sana katika fasihi simulizi ya Waswahili. Kwa mfano Fumo Liyongo, jagina wa Waswahili alikuwa maarufu sana kwa matumizi ya nyuta na mishale. Ni mojawapo >a kazi zilizozungumziwa katika **Desturi Za Waswahili**

## 2 n Matumizi ya miti

ivljti ni muhimu sana katika maisha ya Waswahili. Miti inakuwa na matumizi mengi sana **lcama** vile kutoa mbao, matunda, madawa, ujenzi wa nyumba na vyombo vya majini (majahazi, mitepe, merikebu), kuni za kupikia, usukaji na kutumiwa kutengeneza tembo. Baadhi ya miti ilikuwa - mikoko, mipingo, mipera, minazi, mikorosho, mitomondo, mikwaju, mifenesi, mivinje; mbali na shughuli za kiuchumi, miti ulitumiwa kwa shughuli za kijamii kama vile kufanyia makafara au kupungia mashetani na vile vile majani na mizizi yake ilitumiwa kama dawa. Fasihi ya Kiswahili inatoa istiari zake nyingi kutokana na miti **hii.** Aidha matumizi yake hudhirika katika mashairi, nyimbo, methali, ngano na hata miviga. Kwa mfano katika utenzi wa Fumo Liyongo pametajwa namna shujaa huyu alivyotumia uta na mshale kuangusha makoma.

## 2.18 Uvuvi

Uvuvi ni sehemu muhimu sana ya uchumi wa Waswahili. Uvuvi huu hufanywa mitoni na kwa kiwango kikubwa, baharini. Uvuvi huhitaji mbinu na vifaa mbalimbali. Baadhi ya vifaa vinavyotumiwa ni kama vile mikuki, mitego, nyavu na majahazi. Kuna aina mbalimbali za majahazi - ngalawa, hori, mtumbwi, dau, mtepe na mashua. Mbali na vyombo hivi vya majini, kuna vifaa vingine vinavyotumiwa katika shughuli za uvuvi kama vile pondo, mishipi, migono, madema, munda, kimia na ndoano.

**Isitoshe** kuna aina mbalimbali za samaki kama vile dagaa, kole, jodari sehewa, mkizi, mkundaji, muzia, paragunda, koana, changu, papa, chafi, nguru, taa, mwewe, kamba kole, **pweza,** nyangumi.

**Samaki** ama hutumiwa kama kitoweo au huuzwa ili kuwaletea wavuvi pato, fasihi ya Kiswahili inadhihirisha matumizi ya stiari za uvuvi.

**Kwa** mfano methali - wavuvi wa pweza hukutani mwambani, mgaagaa na upwa hula **waii mkavu,** Hasira za mkizi furaha ya mvuvi. Mashairi, nyimbo na hata ngano hutumia msamiati **wa uvuvi.**

### 2.19 Kilimo

Waswahili hujihusisha na kilimo cha aina mbalimbali. Kuna kilimo cha kuzalisha chakula na **kile** cha kuwaletea fedha. Aidha kuna kilimo cha mboga na matunda. Kilimo cha matunda huhusisha upanzi wa minazi, miembe, mikorosho; michungwa, milimau7, michenza, **mipopoo,** mikoma, michikichi na migomba. Na kwa upande mwingine upanzi wa mimea ya chakula huhusisha; mihogo, nduma, njugu, mtama, mawele, mahindi, mpunga, miwa na **viazi.** Nayo ya mboga ni kama vile, kunde, mbaazi, boga, maharagwe, kisamvi, mchicha.

**Kilimo** mbali na kuwapa Waswahili fedha hutugemewa sana kuwapa ndishe bora ambayo **ni muhimu** kwa afya zao. Isitoshe kilimo huendeshwa kwa vifaa mbalimbali kama vile miundu, **majembe,** viselema na kotama. Uzalishaji mzuri wa mimea hutegemea ufahamu mzuri wa **mistmu** - misimu ya kiangazi, masika na vuli. Shughuli za kilimo hufanyika kulingana na

misimu hii Matayarisho maalumu sharti yafanywe ili kukifanikisha kilimo - kufyeka, kuchoma mabiwi ya takataka, kulima, kupanda, kupalilia na kuvuna. Kuna aina za mashamba kama vile weu na konde.

Hali hii ya kiuchumi ya Waswahili inaonekana katika fasihi. Kwa mfano ngano nyingi huzungumza kuhusu umuhimu wa kufanya bidii kondeni au zawadi za mazao ya kilimo zinazotolewa kwa wenye vipawa fulani katika jamii. Aidha ndishe ya watoto huzungumziwa katika hadithi za watoto. Sehemu hii ni moja wapo ya vipengee vya hatua mbalimbali za maisha ya Waswahili jinsi zinavyodhihirika katika **Desturi za_Waswahili** kazi ya Carl Velten, iliyohaririwa na Lyndon Harris.

## 2.20 Biashara na ufugaji

Waswahili wanajihusisha* katika biashara na ufugaji. Wanafuga kuku, mbuzi, ng'ombe, kondoo, punda, ngamia, bata. Mara nyingi mifugo hawa hulishwa na watoto. Ufugaji ni ishara ya utajiri katika jamii. Mtu aliye na mifugo wengi hustahiwa, isitoshe, mifugo huwapa maziwa yanayotumiwa sana na akina mama na watoto ili kuimarisha afya yao.

Waswahili wamejihusisha katika biashara kwa muda mrefu. Tayari tumeshataja kuwa maingiliano baina ya Waswahili na watu kutoka janibu zingine za ulimwenguni yalitokana na biashara. Waswahili vile vile walifanya biashara wao kwa wao, na majirani wa karibu kama vile Wamijikenda, Wapokomo, Wanyamwezi, Wayao. Kulikuwa na siku maalumu za kuenda sokoni ambazo zilijulikana kwa majina mengi kama vile - gulio na soko. Fashihi

simulizi ya Kiswahili inasimulia biashara na ufugaji. Mashairi, nyimbo, ngano, na malumbano ya utani yalifanyiwa hadharani.

### 2 21 Usafiri na usanii

Usafiri na usanii ni miongoni mwa mambo yanayotawala sana maisha ya Waswahili. Kuna usafiri wa majini na usafiri wa nchi kavu. Usafiri wa majini umesifika sana. Ulihusisha kusafirisha abiria na bidhaa katika sehemu mbalimbali za dunia. Usafiri huu unategemea sana hali ya bahari Hindi, namna pepo zinavyoenda, misimu mbalimbali, aina za vyombo vya usafiri na waendeshaji vyombo hivyo. Waswahili wanaunda vyombo vyao vya usafiri kama vile merikebu, majahazi, mitumbwi, mashua, vidau, mitepe. Vyombo hivi vinaendeshwa na mabaharia wakisimamiwa na nahodha. Lengo la usafiri ni kujishughulisha na biashara, uvuvi, kutembelea jamaa na marafiki, safari za kidini hasa kwenda kuhiji. Mbali na usafiri huu wa majini, Waswahili vile vile wanajihusisha na usafiri wa nchi kavu. Usafiri huu unahusisha kutembea kwa miguu, na kutumia wanyama kama vile punda wanaobebeshwa mizigo au kuwabeba watu, isitoshe mikokoteni na rikwama zinatumiwa kwa usafirishaji wa bidhaa mbalimbali.

Waswahili wanajishughulisha na usanaji na vyombo mbalimbali. Lengo la kusanaa vitu hivi ni ama kudhirisha uwezo wao wa kiujumi kuhusu namna walivyofasiri mazingira yao au kama njia ya kujitafutia riziki. Baadhi ya sanaa hizi ni uchongaji mawe, ufinyanzi, useremala, uundaji wa vyombo vya majini, usukaji, ususi, uhunzi, ufuaji na vitu mbalimbali katika tanuri ya moto. Mawe yanachongwa ili kusaidia katika shughuli za ujenzi na hata baada ya kuchimbwa yanatiwa nakshi ili kuyafanya kuvutia sana. Ufinyanzi unahusisha

**genezaji** wa vyombo ama vinavyotumiwa kuhifadhia vitu au kwa kupika mapishi **balimbali** Vyombo hivi vinatengenezwa kwa ufundi mkubwa kudhirisha umuhimu **kubwa** unaowekewa ujumi katika mwonoulimwengu wa Waswahili. Baadhi ya vyombo ni **kama** vile, vyungu, vikaango, magudulia, mitungi, kasiki, vyetezo na viko. Vyombo hivi **vinatumiwa** kuhifadhia maji, nafaka, vyakula, tumbaku au kuwekea ubani.

**Useremala** kwa upande mwingine unahusika katika kutengeneza samani, milango, madirisha, ngoma mbalimbali (msondo, chapuo, mandondu, kumbwaya na yatari), vichanuo, (vitana), makasha, sanduku, vibweta, mbuzi za kukunia nazi, viatu vya miti, miko, pau, kata, mikongojo, vinyago. Vyombo hivi baada ya kutengenezwa hupigwa msasa na kutiwa nakshi kwa ufundi mkubwa. Sanaa ya useremala inategemea sana zana zifuatazo; shoka, visu, koleo, jiziwa, msumeno, misumari, kekee, parafujo, tupa, jambeni, bisibisi, msasa, chembeu, randa na patasi. Vyombo vinatengenezwa kulingana na mahitaji mbalimbali ya watu ili kurahisisha maisha yao.

Usukaji na ususi unategemea sana malighafi ya kienyeji au wakati mwingine yale yaliyoagizwa kutoka nchi zingine. Baadhi ya malighafi haya ni; pamba inatumiwa kutengeza gora za vitambaa; majani ya miti - minazi - majani yake yanatumiwa kutengeneza fagio, nyungo, mapakacha, pepeo, madema na katika kuezekea nyumba. Mbali na minazi, miyaa (mikoche) na mikindu inatumiwa katika ususi wa mikeka ya kulalia, misala ya kusalia, vitanga na kawa za kutunzia chakula, majamvi, vikapu, shupatu, mbali na ususi unaotegemea majani ya miti, kuna na ususi wa nywele hasa upande wa wanawake kama njia ya towarembesha.

£una na sanaa zingine kama vile kutengeneza viatu, au vifuko vya kuhifadhaia vishale, visu, champali au ndara. Hivi vinatengenezwa kutokana na ngozi za wanyama. Ufuaji hali Icadhalika ni miongoni mwa sanaa maarufu Uswahilini. Kuna ufuaji wa aina mbalimbali Icama vile ufuaji wa vyuma (uhunzi), ufuaji wa fedha, dhahabu (usonara). Ufuaji wa madini haya unafanywa na wataalamu wanaojulikana kama Wajumi (wajume). Vifaa mbalimbali vinatumiwa katika kutekelezia kazi hii. Miongoni mwa vifaa hivi ni kama vile; fuawe, mifuo (mivukoto), nyundo, shoka, koleo, tezo, patasi, juba, bisibisi. Mafundi hawa hutengeneza vyombo au vifaa vya kufanyia kazi, kulimia na mikuki ya uvuvi. Mbali na ufuaji kuwapa Waswahili kipato chao cha kila siku, unawapa nafasi ya kudhihirisha uwezo wao wa kiakili yaani wa kusanii ambayo ni sehemu muhimu ya mwonoulimwengu wao.

Usanii na usafiri ni mambo ambayo yanachukua nafasi kubwa sana katika mwonoulimwengu wa Waswahili. Mambo haya yamezungumziwa kwa mapana na marefu katika fasihi ya Kiswahili. Stiari na taswira zinaojitokeza katika kazi hizi humulikia sana mazingira ya maji na nchi kavu inayopakana na maji. Aidha mambo haya yanatupa nafasi ya kuona namna Waswahili walivyokabiliana na mazingira haya hasa ufanisi, matatizo na jinsi ya kukabiliana na matatizo hayo. Vipengee hivi vimezungumziwa katika **Desturi za Waswahili.**

### 2.22 Mfumo wa Kijamii

Waswahili wana namna ya kuipangilia jamii yao. Mpangilio au mfumo wa kijamii unahusisha mambo mbalimbali kama vile; wanavyoyapangilia makazi yao, familia, koo, ttavazi na urembo, na hatua mbali mbali za maisha yao; kushika mimba, kuzaliwa, mtoto

jcupewa ji[na]> tohara, malezi ya mtoto na mama, elimu, kuoa, kifo na mazishi. Kila hatua ^gmbatana na sherehe maalumu, kuonyesha umuhimu wake katika jamii. Hii ni sehemu muhiniu sana ya mwonoulimwengu wa Waswahili. Ndiyo huwapa utambulisho na upekee **miongoni** mwa jamii zingine.

Chiraghdin (1977: xi) anasisitiza jambo hili anaposema:

> "... Wabantu wa upwa na Afrika Mashariki na visiwa mbalimbali vilivyo jirani ni Waswahili , nao wana kabila zao maaalumu mbalimbali, na ndani ya kabila hizo muna magawanyiko ya vijikabila, na ndani ya vijikabila hivyo muna mbari na koo".

Mtaalamu huyu ametoa mwangaza kuhusu mpangilio wa mahusiano ya kijamii. Kulingana naye, kipashio kikubwa ni kabila na kidogo ni mbari na koo. Jambo ambalo haliko dhahiri kutokana na maelezeo yake ni kama mbari na koo ni kitu kimoja au tofauti. Kazi hii itachukulia familia kama kipashio kidogo kikifuatwa na mbari kisha kabila kitakuwa ndicho kikubwa.

### 2.23 Familia

Familia ni muhimu sana katika jamii za kiafrika. Ndiyo uti wa mgongo wa jamii. Familia huweza kuhusisha mke na mume; mke na mume huyu huungana kupitia kwa ndoa; ndoa nuunganisha familia mbili au zaidi. Kukua kwa familia na hali kadhalika jamii kunategemea sana kupatikana kwa watoto, kuzaliwa kwa watoto nako husababisha kuwepo kwa mahusiano mengine kama vile - Wazazi, babu, nyanya, wajomba, wapwa, shangazi, ami,

rua - mimba, kitinda mimba, mavyaa, bavyaa, wajukuu, umbu, kaka, dada, ndugu, ji. Lengo au uamilifu mkuu wa familia ni kuendeleza kizazi.

\Vatoto wana jukumu la kuwaheshimu wazazi wao kama njia ya kushukuru yote waliofanyiwa na wazazi wao. Fasihi simulizi kupitia kwa vipera vyake vingi ina mafunzo kuhusu hasara au faida watoto walipata kutokana na kuwaheshimu au kuwapuuza wazazi. Kila familia ina filosofia yake ya maisha ambayo kwa kiwango kikubwa inaoana na ile ya mbari au kabila. Hii filosofia ya familia tunaweza kuimithilisha na mwonoulimwengu wa familia hiyo. Kila familia ina mizozo yake, ufanisi wake, imani yake, sherehe zake, namna ya zinavyooana, kuwapa watoto majina, vipengee ambavyo kwa kiwango kikubwa vinamuiika mwonoulimwengu wa jamii hiyo.

### 2.24 Koo na Kabila

Familia kadhaa zikija pamoja huunda mbari au koo. Waswahili walikuwa na makabila kama vile; Wagunya, Washaka, Wapaza, Wasiu, ' Wamvita, Wakilindini, Wajomvu, Wabarawa, Washomvi, Wapemba, Watumbatu, Wamtang'ata, Wangazija, Wamrima, Waamu, n.k. yaliyoenea sehemu mbalimbali za mwambao, wa Afrika Mashariki na visiwa vyake. Ndani ya makabila haya, kulikuwa na koo mbalimbali. Kwa mfano katika kabila la Wabajuni kulikuwa na koo zifuatazo: Shungwaya, Ngumi, Koyama, Tendaa, Twayu, Vekuu, Zitindini, Kiunga, Umbuyi, Omwe, Simambaya, Avutila, Kiliyo, Faradho, Rasmali, Daile, Amshiri, Hartikawa, Upembo, Utanuni, Takwa, Uwani, Vumwe, Kisimayu, Birkao, Ndipingoni, Kiwayuu, Dili, Vero na Mvivi.

jsjao Waamu walikuwa na koo zifuatazo: Famao (Famao - Weli na Famao - Nafasi), VVayunibili, Kinamte, Waungwana wa Yumbe, A1 Bakari, A1 Bereki, Bashekh, Miraj, Almawii (al-Bauri), A1 Madi, Jahadhmy, A1 Husseini na A1 Ahdah.

]^ao Wavumba wana koo zifuatazo: Ba Amiri, Ba Alawi, Chifundi Changani, Muyani, \fbayanyi, Kirui, Uso, Ulenge na Paji.

Asili ya Waswahili ni kuhesabu ukoo kukeni. Fahari ya Nf swahili iko kwa mama wala si kwa baba. Waswahili hawapingi kuolewa na wageni au wasio Waswahili, maana kuolewa na watu walio kando ya kabila hilo huwa hukuathiri mila yao wala kizazi chao kwa sababu mtoto azaliwaye huwa si wa kabila la mume wa kigeni bali ni wa kabila la Kiswahili. Tokea zamani watukufu wa miji ya Waswahili, pepo wao, watukufu wao wamekuwa na majina ya kike - kina Mwana Chambi, Mwana Mkisi, Mwana Mtwapa, Mwana Upatu n.k. Chiraghdin (1977: x).

Kuelewa barabara mwonoulimwengu wa Waswahili ilikuwa muhimu kuielewa mahusiano. Jinsi nadharia ya kazi hii inavyoeleza; kila kitu, hatua, mahusiano na sherehe yalikuwa na uamilifii muhimu katika jamii. Na ni uamilifu huu ulioelezea ulimwengu wao.

### 2.25 Dini, itikadi na uchawi

**Waswahili** kama walivyo waafrika wengine wana na imani na itikadi. Imani na itikadi ni muhimu katika kuwapa moyo wakati wa misukosuko na misiba, kuelezea 'mazingaombwe' wanavyokumbana nayo katika maisha yao. Pana na haja ya kupatana na Mungu au Miungu rti kuiepushia balaa au kutafuta uombezi wakati wa shida. Maisha licha ya kuwa na nyakati

. e ^ furaha yanakuwa na hatari zake ndipo miko ikawekwa na matambiko mbalimbali ku&nywa Sehemu nyingine ya imani na itikadi ambayo ni muhimu kutajwa ni imani katika wafu Wafu walistahili kutunukiwa heshima, la sivyo wangeweza kuiletea jamii mikosi na misiba isiyohesabika.

**Mwonoulimwengu** wa Waswahili wanadhihirisha sifa hizi za kiimani na kiitikadi. Licha ya Uislamu kukita mizizi miongoni mwa Waswahili ni vigumu sana kuweka mpaka baina ya imani za kidini na ushirikina. Utata huu unadhihirishwa na Muhammad S. Farsy (1960: 3) anaposema:

> " ... Hadithi iliyoandikwa katika kitabu hiki ni ya kubuniwa tu, nayo imeandikwa kwa madhumuni ya kujaribu kueleza namna watu wanavyoishi katika vijiji vyetu. Haya yamefanywa kwa kusudi la kuhifadhi baadhi ya mila zetu ... maana mengi kati yale tuliyoyaeleza hayafanywi tena ... Nitapenda kuwatanabahisha wasomaji wangu kuwa nyingi katika ada na desturi nilizozieleza hufatanishwa na mambo ya dini >na kudhaniwa kuwa kuwa ni dini; hayo ni makosa makubwa maana ada na desturi hizo ni za kikafiri ni dhambi kubwa sana kuzifuata".

Mtaalamu huyu ambaye yeye mwenyewe ni Sheikh wa dini ya Kislamu anajipata katika njia panda. Upande mmoja anatambua umuhimu wa desturi za Waswahili ambazo anahofia zinapotea na huenda zikasahaulika kabisa na vizazi vya sasa na vya siku zijazo. Mtaalamu ^yu alichukua hatua ya kutunga hadithi kama njia ya kuzihifadhi na vile vile "kuwasaidia wana wa vyuoni na wanafunzi waliohusika na masomo ya tabia na hali za watu." Isitoshe,

**alitambua** umuhimu wa desturi hizi kufundishwa na kufanyiwa utafiti katika vyuo vikuu. iman* inamfanYa 'kujikosoa'. Mashehe wetu ... wanafanya jitihada kuu Icuyakataza kwa kuyapigia makelele katika magazeti, maredio na mihadhara ya watu.

Waswahili wote wawe Waislamu na wasio waislamu wanaamini kuwepo kwa mikosi na **uchawi** ambao unaweza kuombewa dua. Mbali na haya kuna imani katika pepo, mashetani na majini. Inaaminika kwamba pepo hawa huishi mizimuni. Mikosi huweza kuepukwa kwa kutoa kafara au kufanya matambiko. Kafara hizi zaweza kufanywa na mwalimu wa kidini au mganga. Isitoshe, watu huvaa hirizi za aina mbalimbali kama vile: hirizi ya vita, na ya uvuvi. **Kwa** hivyo watu, wanyama, mimea, makazi, biashara vyote hivyo vinaweza kukingwa na balaa kwa kutumia hirizi. Wale waliostawi kiuchumi husemekana kuwa wana majini. Majini huweza kutumiwa kuwaletea wapinzani balaa ili wasitoe ushindani katika biashara.

Itikadi, imani na uchawi vile vile imetawala fasihi ya Kiswahili. Kuanzia kwa kuzaliwa hadi kifo. Chochote kinachojiri huhusishwa na ushirikina. Kwa mfano, mwanamke asiposhika mimba husema amerogwa au ulemavu wa aina yeyote ite huhusishwa na ushirikina.

### 2.26 Namna Waswahili wanavyoelezea Mwonoulimwengu wao

Waswahili wana namna yao ya kuelezea mwonoulimwengu. Chraghdin akinukuliwa na Noor Shariff (1988: 8 - 9 ) anasema:

> "... Ikiwa kabila ni watu wenye lugha maalumu na fasihi iliyotaalaki na mawazo na maliwazo ya watu hao, tamaa zao na utu wao basi lugha hiyo, yaani Kiswahili, ina mambo hayo na ni chombo kinachowatumikia watu

wenye haya kama hizo tokea kale - ngano zao, nyimbo zao, mashairi yao na mitindo mingine ya tungo mbali mbali zikawa ni za mapokezi au za maandishi

jsli dhahiri kutokana na maelezo haya kuwa mwonoulimwengu unaweza kuelezewa kwa njia mbalimbali. Baadhi ya njia zimetajwa na Chiraghdin. Njia kuu aliyoitaja ni fasihi ambayo licha ya kutumiwa kama kioo cha jamii, inashirikishwa kikamilifu katika maisha ya Waswahili. Fasihi inatumiwa kuwaliwaza, kuwaburudisha, kuwakumbusha kuhusu majukumu na sheria za jamii. Utanzu unaojulikana zaidi ni ushairi. Mashairi yalitungwa katika hati za kiarabu. Hata hivyo, utamu wa ushairi haupatikani katika kuandika, bali katika usimulizi na uimbaji. Ndipo yakaibuka mashairi ya kila aina - tenzi, tarbia, tumbuizo, ngonjera na takhmisa.

Mbali na ushairi, utamu wa nathari vile vile unaitumiwa kuelezea mwonoulimwengu wa Waswahili. Jack Rollins (1983) na Rajmund Ohly {1981) wameziainisha tanzu hizo za kinathari. Ohly akitumia sana kigezo cha maudhui ameibuka na kategoria zifuatazo: -

(i) Nathari ya kihistoria - Mifano ni kama vile Habari za Lamu, **Habari za_Pate, Habari za Wakilindi, Uhuru wa Watumwa, Adili na Nduguze, Kufikirika.**

(ii) Nathari ya Kiethnografia - mifano kama vile mikusanyiko ya Carl Velten - **Desturi za Wasuaheli** (Ambayo inahikikiwa katika kazi hii), **Ada za Harusi katika Unguja, Kurwa na Doto.**

(iii) Nathari za safari - Safari za Wasuaheli, **Tulivyoona na Tulivyofanya Ingereza, Shamba la Ushirika.**

(iv) Nathari za mafundisho - nathari hii inahusisha ngano na hadithi za kitamaduni za kale ambazo zilikuwa na mafunzo ama yaliyo wazi au yaliyokuwa yamefichika. Baadaye zilianza kuingia katika uandishi wa nathari. Mifano ni kama vile; - Masomo yenye Adili, **Jihadhari na_wake wa watu, Titi la Mkwe, Safari ya Ndoa Saba.**

(v) Tawasifu na Wasifu - mifano; Maisha ya Hamed bin Mohamed el-Murjebi, **Maisha ni kitu Aali.**

(vi) Nathari za Tafsiri - kwanza zilifanywa na wazungu na baadaye zikafanywa na Waafrika wenyewe. Mifano iliyotolewa ni: **Maisha yenye Maana, Masimulizi ya Afrika.**

Rollins kwa upande wake alipata tanzu zifuatazo za kinathari: Tarihi, Kumbukumbu, Tawasifu, Kisa, Hadithi, Hekaya, Habari, Kioja, Wasifu, Simo, Masimulizi, Neno la Hekima, **Ngano.** Tarihi zinazojitokeza katika uanishaji wa Rollins ni kama vile: **Tarihi_za Kilwa, Pate, Vumba, Mombasa, Shungwaya, Habari za Wajomvu, Habari za Mrima, Habari za Wakilindi.** Mifano ya kumbukumbu na Tawasifu ni kama vile: **Safari Yangu na Bara Afrika, Safari Yangu ya Urusi na ya Saiberia.** Vile vile katika sehemu hii ameorodhesha mikusanyiko ya Edward Steere, Carl Velten, Bultner, Burton na **H. P.** Blok. Kazi hizi zote zinaelezea mwonoulimwengu wa Waswahili.

Mwonoulimwengu wa Waswahili vilevile unaelezewa katika mavazi na mapambo, muziki na densi. Baadhi ya mavazi ni kama vile Kaniki, Shihiri, Kibuti, Leso, Dusmali, Ukaya, **Barakoa.** Wanawake hali kadhalika walijipamba mapambo ya dhahabu na fedha, diwi, hazama, kisharafa, yasi, pingo ya kiasi, kipini, majebu, dodi, kunga, ishoe. Wanaume nao walivaa vikoi, shuka au doti, kanzu, kofia (kofia ya kibandiko, sina, hasara, bandi, wimbi, mtama, darizi, juba, bushuti, kilemba, mkumbuu na joho). Aidha walitembea wakitumia bakora au henzerani zilizonakishiwa vizuri. Mavazi mbali na kufunika uchi, yalitumiwa kuwarembesha. Hii ni ishara kwamba Waswahili walithamini ujumi.

Waswahili pia wana muziki na densi zao zilizo na uamilifu mbalimbali katika jamii hii. Muziki na densi hudhihirika wakati wa kusali, kuburudika au kujiliwaza wakati wa majonzi. Densi hizi hujulikana kama ngoma. Ngoma huchezwa kwa ala maalumu. Kulikuwa na nyimbo kama vile za gungu, diriji, lelemama, vave, msapata, tari, nyimbo za waganga na nyimbo za ziyembe. Kati ya nyimbo au ngoma hizi gungu ndiyo iliyojulikana sana. Fumo Liyongo alikuwa stadi wa kucheza gungu. Ngoma hu&ndamana na ala mbalimbali za muziki kama vile: Ngoma kadhaa: vuwe, chapuo, mshindo, msondo, tutu, rewa, kindimba, kiminingo na mrungura; ala zingine ni: tari, kinganga, gambusi, kinanda, siwa, baragumu au gunda, chuku, kikasiki, ndumiko, zumari, kayamba, miwale, sariji ya cherewa, misewa, njuga, upatu, marimba.

assa*''''88®

J0MO KENYATTA MCMQRIAI

## 2.27 Hitimisho

Sura hii imejaribu kufafanua dhana ya mwonoulimwengu kwa kuelezea elementi zake mbalimbali. Na katika kufanya hivyo imebainika Waswahili wana mwonoulimwengu wao. Aidha tumejaribu kuelezea upana wa utamaduni wa Kiswahili ambao kimsingi ni wa kibantu lakini una athiri kutoka kwa Uislamu. Usimilishaji huu wa Uislamu katika utamaduni wa Kiswahili, umechangia pakubwa kukuza utamaduni wa Kiswahili. Na ni utamaduni huu unaotupa mwanga kuhusu namna Waswahili walivyoufasiri na kuuelezea ulimwengu wao.

# SURA YA TATU

## XJHAKIKI WA DESTURI ZA KISWAHILI

### 3q Utangulizi

Sura hii itashughulikia uhakiki wa **Desturi Za Waswahili** kazi iliyokusanywa na Carl Velten baina ya mwaka 1893 na 1896 na kuhaririwa na Lyndon Harries (1964). Sura hii itaangazia kuhusu ukusanyaji na uhariri wa kazi, uhakiki wa hatua mbalimbali za maisha mkazo ukiwa kwenye hatua zifuatazo: kushika mamba na kuzaliwa, mtoto kupewa jina, malezi yake, tohara na elimu, ndoa na kifo. Uhakiki wa kazi hii utakuwa unachunguza elementi mbalimbali za mwonoulimwengu wa waswahili zinazojitokeza katika hatua hizi. Baadhi ya elementi zitakazoangaziwa ni kama vile; kinga dhidi ya hatari, ushindi au kufaulu, matumizi mabaya yamadaraka, vidhibiti, dhidi ya matumizi mabaya ya uwezo, ujumi, kutegemeana baina ya kifo na maisha, ujamaa na uendelezaji wa kizazi, utakaso, usababishi wa misukosuko, usambazaji na uhifadhi wa maarifa, afya, utabibu, ndishe, ushujaa, uvumilivu na nguvu ya sala.

### 3-1 Ukusanyaji na uhariri wa desturi za waswahili

^i hii ni mkusanyiko wa Carl Velten uliofanywa baina ya mwaka 1893 na 1896. Mkusanyiko huu uliandikwa na Mtoro bin Mwenye Bakari akisaidiwa na Selemani bin Mwenye Chande, Salim bin Abakari na Abdallah bin Rashid. Mtoro bin Mwenye Bakari

jiandika kazi hii akifanya kazi ya ukalimani katika serikali ya kikoloni ya Kijerumani jsjchini Tanganyika. Kazi hii ilieleza desturi za waswahili wanaoishi sehemu ya Mrima yaani \yamrim[a]

Lyndon Harries katika utangulizi wa **Swahili Prose Text** anatuelezea ya kwamba, baada ya Carl Velten kufanywa Profesa wa Kiswahili katika "Institute of Oriental Languages", chuo kikuu cha Berlin, mwaka wa 1896 ndipo dhana ya kuchapisha kazi hii ya Mtoro bin Mwenye Bakari iliyoandikwa katika Kiswahili iliponjia **Desturi za Wasuaheli** ilichapishwa mnamo mwaka wa 1903 ikitanguliwa na kazi nyingine ya mwandishi huyo; **Safari Za_WasuaheIi** mwaka wa 1901. hizi kazi mbili zilihaririwa upya na Lyndon Harries mwaka wa 1964 na kuziita; **Swahili Prose Tests,** Harries aligawa kazi hii katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ilihusu desturi za waswahili na ya pili Safari za Waswahili. Harries anaelezea katika dibaji sababu za kuhariri upya kazi hizi za Carl Velten:

> "... Vitabu hivi vyote viwili hupatikana kwa shida sana siku hizi, lakini kwa vile vilivyo na faida nyingi kwa mwanafunzi wa lugKa hii na kwa mwanafunzi wa historia tumeona inafaa kutengeza vipya habari hizo zilizoelezewa na kuandika tafsiri yake kwa Kiingereza pamoja na maelezo ya maneno magumu. ... Habari hizi zina maana sana hasa kwa wasomaji wetu wa Kiafrika, kwa sababu zimehifadhi madhahebu yale ya zamani ya Kiswahili na taratibu zake. Mambo haya yaliyomo humu hayapatikani kuelezwa katika vitabu vingine ... kawaida za maandishi yake zimebadilishwa kidogo katika toleo hili la kitabu makusudi kuzisawazisha na kawaida za maandishi za siku hizi."

£ulingana na mtaalamu huyu, kazi hii ilikuwa muhimu sit u wanafunzi wa fasihi na historia bali kwa kila mtu hasa wale walio na hamu ya kufahamu maisha ya waswahili haza wonoulimwengu wao. Jack Rollins **(1983: 58-59)** anaisifu kazi hii kuwa ya kiwango cha **juu zaidi** inayoelezea maisha ya waswahili wa eneo la Mrima katika miaka ya **1890.** **\ltaalamu** huyu anasema ya kwamba, **Desturi za Waswahili** ni kazi inayoweka bayana **utambulisho** wa kitamaduni wa waswahili. Akiilinganisha kazi hii na ile ya Maisha ya Tippu Tip, Rollins anaungama kuwa, kazi hii inadhahirisha wazi mila za waswahili.

**Hata** zile mila za asili ya Kiarabu kama vile sherehe ya **Akika** zimesimilishwa katika **utamaduni** wa Waswahili. Katika kuhitimisha, mtaalamu huyu anaungama ya kwamba, Desturi **za Waswahili** ni kazi inayoshughulikia kwa mapana na marefu kuzaliwa, ndoa na **kifo.** Mbali na hatua hizi muhimu za maisha, kazi hii vilevile inaelezea kuhusu tohara, elimu ya kiislamu, peop, ngoma, viapo, ushuru, magonjwa, talaka, magonjwa na kadhalika.

**J. de** V. Allen akinukuliwa na Rollins **(1983: 59)** vile vile anaisifu kazi hii kwa kuiona kama ni mwongozo wa kuuelewa utamaduni wa waswahili. J. de V. Allen anaungama ya kwamba, mada ya kazi hii ni dhihirisho tosha la kuwepo kwa jumuia ya waswahili.

### Hatua mbalimbali za maisha jinsi inavyojitokeza katika desturi za Waswahili

**Desturi** za waswahili ni kazi inayojikita upande wa hatua mbalimbali za maisha ya waswahili, yaani kuzaliwa, ndoa na kifo. Kila hatua huchukuliwa kuwa muhimu zaidi katika **maisha** ya waswahili. Hatua hizi huonyesha kukua na kubadilika kwa maisha ya watu hawa. Kila hatua huambatana na sherehe maalumu. Katika sherehe hizi hutolewa kafara,

.alT1biko yakafanyika viapo na sala vilevile kufanyika. Isitoshe nyimbo huambatana na shughuli hizi. Yote haya hufanywa ili kusherehekea ushindi au ufanisi kwa mfano wa mtoto l^aliwa, kuoa au kuolewa; kinga dhidi ya pepo waovu, magonjwa na mikasa mbalimbali. jviambo haya hutupa picha kamili kuhusu mwonoulimwengu wa waswahili. Kusimbua **maana** ya sherehe na shughuli hizi huhitaji ufahamu wa hali ya juu ya utamaduni wa waswahili. Chochote kinachofanyika huwa na uamilifu mahususi katika jamii hii.

**Carl** Velten katika **Desturi za Waswahili** ameigawa kazi hii katika vijisehemu mbalimbali,

(i) Mtoto mchanga-katika sehemu hii amejishughulisha na;Akika/kuzaliwa kwa mtoto, kumwonyesha mtoto jua na mvua, kumnyoa mtoto kwa maulidi.

(ii) Ulezi wa mtoto-sehemu hii imeangazia-ndishe na afya ya mtoto,majina ya mtoto, kuota meno, kumzingua mtoto mgonjwa, chale za malole, kumlea mtoto aliyefiwa na mamake, mtoto wa mazeru, kwenda chuoni, kuwarudi watoto, elimu ya watoto, adabu za watoto, kumtia mtoto kumbini, kuwarejesha wari majumbani kwao, mtoto mwari, kuvunja ungo, wari katika kumbi lao, wari kupelekwa muyomboni na kurudi kwa.

(iii) Habari ya kuoa-sehemu hii inajishughulisha na maposo, kikombe cha kahawa, kupiga pamba, siku ya harusi, fungate, mwisho wa harusi.

(iv) Kazi ya kawaida-kulima shamba, matumizi ya mnazi, safari ya kwenda bara, wasiopenda kusafiri, wanyamwezi wajao Pwani, Amri ya jumbe, Biashara ya utumwa, kuvua samaki, kuunda jahazi, kazi za wanawake, kusukana nywele, uzuri wa wanawake, kazi za mikeka.

(v) Mambo ya mjini-Habari ya majumbe, mali ya jumbe, siku kuu ya koga, Habari ya Ramadhani, Idi kubwa, Ngoma za furaha, Habari za pepo, Namna za pepo.

(vi) Kawaida ya utumwa- asili ya utumwa, kazi za watumwa, adabu ya mtumwa, nikaha za watumwa, Habari ya masuria, mtumwa kuwekwa rehani, hati ya uhuru.

(vii) Mambo ya sheria-vifungo vyetu vya zamani, magereza, Habari ya viapo, Mashtaka makubwa, Sheria ya wizi, Sheria ya deni, desturi ya bei, kuweka rahani, Habari ya talaka.

(viii) Maziko- Habari ya matanga, Kufa kwake Jumbe, Kuhalilia Mbwe.

Tasnifu hii itaangalia hatua za kuzaliwa hadi hatua ya ndoa. Katika kuzielezea hatua hizi tutaanzia katika kuzaliwa, mtoto kupewa jina, malezi ya mtoto, elimu ya mtoto, tohara, ndoa, utenda kazi katika jamii, kifo na mazishi. Aidha tutajadili dhana ya pepo, ngoma na sherehe mbalimbali za waswahili.

## 3.3 Kuzaliwa

Kuzaliwa kwa mtoto hi kiungo muhimu cha familia na jamii kwa jumla. Familia ni kitu muhimu katika jamii za Kiafrika. Ndiyo msingi wa maisha na hali kadhalika uti wa mgongo wa jamii. Bila familia hakuna jamii. Familia ndiyo kiunganishi baina ya mtu na Mungu wake. Familia huhusisha baba, mama, wajomba, shangazi, ndugu, dada, wapwa, ami, watoto na jamaa wengine wote. Kwa hivyo kila mtu huishi, hufa na kuzikwa mahali alipozaliwa kwa kuzingatia mila za jamii hiyo.

wa ^ P 3 ^ watoto ™ jambo muhimu kwani kuzaliwa kwa watoto ni dhihirisho la **j^endelea** kwa jamii hiyo. Kuzaliwa ni hatua inayowapa watu hakikisho kwamba familia, tyazi, jamii au maisha ya siku za usoni yameshughulikiwa. Kulingana na John S. Mbiti (1969: 110) uzazi ni tukio muhimu si tu kwa wazazi bali jumuia nzima. Maumbile humleta mtoto huyo duniani lakini jamii ndiyo humkuza hadi akawa mshirika kamili la kumlinda nitoto, kumlisha, kumkuza na kumuelimisha. Ndiposa katika jamii nyingi za Kiafrika, mtoto **husemekana** kuwa wa jamii na wala siyo wa mtu binafsi.

Uzazi ni mchakato unaoanzia katika mume na mke kuoana. Kuoana kwa mume na mke huleta pamoja familia mbili au zaidi. Muungano huo hudumisha tu iwapo mtoto atapatikana. Ndoa huwapa hawa wawili mamlaka ya kujihusisha katika ngono - kitendo kinachohitajika ili watoto wapatikane. Baada ya kitendo hiki mwanamke alitarajiwa kushika mimba. llikuwa hatia au kasoro kubwa iwapo kutoendelezwa hangeshika mimba. Kutoshika kulimaanisha kutoendelezwa kwa kizazi. Hali hii ili'fasiriwa kama laana au mkasa wa kijamii.

Maandalizi kabambe yalistahili kufanyika kwa kuilea mimba na vilevile kwa shughuli ya kujifiingua.

**katika** kazi hii ya **Desturi za** Waswahilijunnaelezwa kuwa Mama mja mzito alilishwa Vlzuri ili kuiboresha afya yake na hali kadhalika ya mtoto aliye katika tumbo la uzazi. Mama ^yelishwa vizuri angepata taabu wakati wa kujifungua kwa kukosa nguvu za kumzaa mtoto.

^jdha vyakula tofauti tofauti vyenye uamilifu mbalimbali vilikuwa muhimu kumsaidia jaijTikuza mtoto aliye na afya nzuri. Isitoshe, mama huyu alistahili kulindwa kutokana na hatari yeyote kwa mfano kujiweka baidi vitu ambavyo vingemdhuru. Kwa mfano tunaambiwa kuwa mama mja mzito hakupitiwa na mtu aliyechukua moto, wa kama chochote gnibacho kingeweza kumdhuru mama mjamzito.

Moto ni stiara ya nguvu zozote haribifu. Wanaweza kuwa pepo waharibifu, vifaa viharibifu au mahasidi waharibifu ambao wangeweza 'kuukata uzazi' yaani ambao wangeweza kumfanya mama mjamzito kutojifungua salama salimini.Maandalizi hayakukomea hapo, palihitajika maandalizi mazuri kufanywa kwa ajili ya kuzaliwa kwa mtoto hasa vifaa mbalimbali vilivyohitajika kwa shughuli hii.

Kulingana na Farsy (1960)hatua ya kuzaliwa ilikuwa shughuli muhimu isiyopaswa kuchezewa sharti pawe na maandalizi yanayofaa. Kila siku inapokatika, hali ya wasiwasi na hamu huzidi. Mama mjamzito huombewa dua na kupewa moyo na jamaa pamoja na marafiki. Hata siku ya kujifungua inapokaribia, mama mjamzito huanza kuumwa na tumbo la uzazi. Wakunga hualikwa kuliuguza tumbo. Isitoshe, mwalimu wa dini hualikwa kuomba dua. Hapa tunaona ya kwamba, licha ya kuhitajika kwa wataalamu wa juzalisha (wakunga), panahitajika dua. Kwa hivyo sala zina nguvu. Ndizo humfanya Mwenyezi Mungu kuepusha maovu, kama vile kifo cha mtoto au mama, kuzaliwa watoto walio na ulemavu - makengeza, zeruzeru, vipofu, kiguru n.k. Aidha sala huteremsha uwezo wa Mwenyezi Mungu kusahilisha uzazi. Pale wakunga wanaposhindwa, humtegemea Mungu.

jehemu hii inadhihirisha uwezo mkubwa aliopewa Mwenyezi Mungu katika nvvonoulimwengu wa waswahili. Licha ya imani katika ushirikina, waswahili wanaamini ^vva uwezo wa juu zaidi unatokana na Mungu ambaye anaweza kufikiwa kupitia kwa sala. lambo lingine la muhimu la kutaja hapa ni kwamba, tunaona mwingiliano mkubwa baina ya jtamaduni asilia wa Kiswahili na uislamu. Mambo haya mawili huenda sambamba.

£wa msaada wa wakunga, mwalimu, sala za jamaa na marafiki mtoto huzaliwa. Kuzaliwa cwa mtoto huandamana na sherehe muhimu. Sharti mtoto huyu afanyiwe mambo nbalimbali kabla ya kukabidhiwa jamii rasmi. Mtoto sharti akokegeshwe na mama cutengenezwa kabla ya baba wa mtoto kuruhusiwa kumwona mtoto na mkewe. Ada zote jharti zifuatwe. Tutazizungumzia kwa kirefu ada hizo. Lakini mwanzoni kitoto cilichozaliwa hufungwa vigwe, mvunje na nyimbili. Jufunguliwa koo kwa kurambiswa asali 1a shubiri; hurembwa muru na wanja mikononi, miguuni na usoni. Aidha kitoto hulazwa idani ya nyungo za mchele, zenye chuma na kaa. Shimo huchibwa nyuma ya nyumba na citovu cha mtoto huyo huzikwa pamoja na makaa, chuma na chumvi. Kabla hakijafukiwa, titovu hiki kilifudikizwa kijungu kipya tena kikafunikwa na kabla shimo halijajaa vizuri, unazi mchanga hupandwa katika shimo hilo. Wakati mambo yote haya yakiendelea, vyetezo luhanikiza moshi wa ubani katika nyumba.

Inabidi mtoto afanyiwe haya yote ili kumkinga kutokana na hatari mbalimbali. Hatari kuu luwa ni ile inayoweza kusababishwa na pepo waovu au mashetani kwa hivyo vigwe, Mvunje, kurembwa wanja na muru, kufuka kwa moshi wa ubani hunuiwa kuwafukuza pepo 1a mashetani wanowezataka kumnyemelea mtoto aliyezaliwa. Kurambishwa asali na shubiri

^ namna Fulani ya misukosuko na furaha. Asali ni stiari ya furaha, ufanisi wa maisha ambao mwanadamu hukumbana nayo. Shubiri ni stiari ya misukosuko au matatizo mbalimbali ambayo binadamu hukumbana nayo. Kwa hivyo misukosuko licha ya kwamba ni 'michungu' kama ilivyoshubiri, sharti ivumiliwe wakati ikitafutiwa suluhisho. Mtoto awe tayari kupitia hizi sura mbili za maisha.

Kitovu ni stiari ya asili au usuli wa jamii au kizazi na huhifadhiwa mchangani kuonyesha walipoanzia wanadamu na watapoishia. Kupandwa kwa mnazi ni kumbukumbu ya asili ya jamii na kuendelea kukua. Yaani kila mtu ana asili yake. Kukua kwake vizuri kunategemea utunzaji na ufahamu mzuri wa asili hii. Na sasa tuzingatie ada zingine zinazofuata baada ya mtoto kuzaliwa.

**3.4 Ada ya akika**

Ada hii ina asili yake kutoka utamaduni wa Kiarabu lakini waswahili wameifanya kuwa yao. Mtoto hufanyiwa ada hii akifikisha miaka saba. Shefehe hii mara nyingi huongozwa na mwalimu wa kidini ambaye huja kuongoza maulidi au kumba dua. Mbuzi wawili huchinjwa ikiwa ni mtoto mvulana na mmoja akiwa ni msichana. Mbuzi mmoja hukaangwa na akaliwa na wali ilhali watu hukaribishwa katika sherehe hii na hushiriki katika ulaji wa vyakula vilivyoandaliwa. Mbuzi wa pili huchomwa kwa mishikaki akaliwa pamoja na asali ya nyuki. Mifupa ya mbuzi huyu hufukiwa udongoni. Inaaminika ya kwamba mifupa hii itatumiwa na Mwenyezi Mungu kumuumba ngamia atakoyetumiwa na mtoto kukwea hadi mbingu ifikapo Siku ya kiama.

**gl^ehe** **hii** ya **Akika** ni ya muhimu tena ya lazima kwa mtoto yeyote anayezaliwa. **Ni** jazima afanyiwe akiwa mdogo na wazazi wake. Na akifika utu uzima kabla hajafanyiwa ni **sharti** aifanye yeye mwenyewe Hata mtoto akifariki ni sharti afanyiwe sherehe **hii.**

**Ada** ya **Akika** inadhihirisha umuhimu mkubwa unaohusishwa na kuzaliwa kwa mtoto. Kuzaliwa kwa mtoto huambatana na majukumu mbalimbali. Mtoto huyo ni lazima **aandaliwe** ili aweze kuishi vizuri katika jamii. Yeye ni mali ya jamii. Ndiyo maana watu **hualikwa** katika sherehe ili wafurahie ufanisi wao. Aidha mtoto huhitaji kuandaliwa kwa maisha ya siku za usoni hasa baada ya kifo chake. Wakati wa kiama mtoto atakaxwe kwa kuombewa dua na kafara kutolewa. Kutotimiza sheria hii muhimu huweza kuleta **balaa** au kisirani katika jamii. Ada ya Akika inaangazia vilevile kuhusu elementi muhimu ya mwonoulimwengu wa waswahili ya kuendelea kwa maisha hata baada ya kifo. Kifo ni ngazi au hatua mojawapo katika maisha.

Stiara ya mifupa ya mbuzi kubadilishwa na kuwa ngamia ya kukwelea hadi mbinguni ina athari za kiislamu. Hii ni stiari ya mchakato mzima wa maisha ya mwanadamu. Ugumu wa mifupa unaweza kulinganishwa na misukosuko inayozuka katika maisha inayohifaji roho ngumu, au uvumilivu wakati ikitafutiwa suluhisho. Upeo wa maisha ya mwanadamu ni kwenda mbinguni. Safari hii ya mbinguni tunaona ikitegemea msaada wa wanyama - ngamia. Huyu ngamia tunaweza kumlinganisha na yule farasi - al-Buraki, aliyetumiwa ma Mtume Muhammad hadi Mukadasi.

## 3 5 Mtoto kutolewa nje

Dhana ya mtoto kutolewa nje humaanisha kumkaribisha mtoto rasmi duniani. Makaribisho j^yo huhusisha kumjuvya kuhusu mambo mbalimbali atakayopitia wakati wa kuishi kwakw. \lambo haya yaweza kuwa mazuri au mabaya, magumu au sahili. Kumtoa nje mtoto huanza baada ya siku saa za kuzaliwa kwa mtoto huyo. Mtoto hupelekwa nje kuonyeshwa jua Tukio hili huambatana na sherehe maalum inayojulikana kama KISINGIZI. Sababu za kuitwa kisingizi ni kwamba wakunga walikosa usingizi usiku kucha wakimshughulikia mama mzazi wakati wa kujifungua. Sherehe ya kisingizi huongozwa na kungwi mkuu ambaye humuuliza baba wa mtoto kutafuta jogoo wa kuchinjwa na kuandaliwa kitoweo ambacho kitaliwa kwa wali. Nguo hutandikwa kwenye kizingiti cha nyumba, kungwi humpakata mtoto kisha akaja mwanamke mzee akiwa ameushika mchi na akaanza kusema na yule mtoto.

## 3.6 Wosia

Mwanamke mzee hutoa wosia kwa njia ya kiapo. Inaarhinika ya kwamba, wakati huu bongo za mtoto huwa tupu zikusubiri kunasa chochote kinachotokana na mazingira mapya. Wosia huo hutamkwa hivi: -

> "… Mungu amekuleta ulimwenguni, shinda moyo wako, na vitu vya watu usiwe mtamani, umekuja ulimwenguni, ziba masikio yako usisikilize maneno ya watu; umekuja ulimwenguni, usiwe mgomvi ukagombanisha watu, kwa sababu wahenga wamesema, lifaalo kueleza lieleze, lisilofaa limeze; umekuja ulimwenguni, usipite nyumba zenye wake wa watu, utapoteza roho yako. Mungu amekuleta katika dunia,

ukae kwa heshima na watu, kwa sababu wahenga wamesema, mwiza mwiza si utumwa."(Uk 3-4)

Kama inavyodhihirika, wosia huu umekaririwa kwa ufundi wa hali ya juu sana. Mbinu ya takriri ikitoa msisitizo juu ya maadili anayopaswa kujifunza na kufuata maishani ili mtoto huyu awe na maisha marefu yaliyo na amani na ufanisi. Na katika kuiandama njia nyoofii adilifu, kuna mambo kadhaa mtoto hastahili kuyatenda. Umri mpevu wa mwanamke mzee anampa nafasi ya kuzungumzia kuhusu maisha kwa mapana na marefu kwa sababu ana tajiriba mwanamke amepewa hadhi kubwa. Tayari tumeshataja katika sura ya pili kwamba nasaba au ukoo uswahilini huhesabiwa kukeni. Hapa mwanamke anaweza kumthilishwa na udongo wenye rotuba nyingi ambao huzalisha chakula kingi (watoto) pindi mbegu zikiatikwa. Kwa hivyo mwanamke ndiye chemi chemi ya maisha. Si hayo tu, mwanamke ndiye huwa mlezi mkuu wa mtoto; ndiye humuongoza mtoto maishani mwake.

Maadili yanayojitokeza katika wosia ni kama vile: - Uvumilivu,Ukinaifu,Kuwa na msimamo,Heshima,Kusema mambo ya kweli

Mambo yaliyokatazwa ni kama vile: -Tamaa,Wizi,Ukware wa kutamani wake za watu,Usabasi,Ugomvi na vurugu,Kusema mambo ya uwongo au yasiyofaa

Mtoto anayekiuka wosia aliyopewa huwaletea wazazi wake aibu na yeye mwenyewe hufedheheka au hata akapoteza maisha.

^akati mzee akiyakariri maneno haya huwa amemuekea mtoto mchi juu ya kifua chake. Stiara yam chi humaanisha mtu anastahili kuwa na moyo mzito kama wa mchi, wa kuhimili vishindo vyote vya maisha. Moyo unatarajiwa kuwa imara wakati wote. Baada ya wosia wa yule mzee, mtoto hutolewa uwanjani akadakwa mara saba akiambiwa atazame juu. Halafu hurejeshwa ndani. Mle nyumbani mtu mmoja humpakata mtoto na mwingine hutia maji katika ungo kasha humnyunyizia mtoto maji hayo huju akitamka: "Mvua, Mvua! Maana jua umeliona nah ii ndio mvua "

Kumrusha mtoto juu mara saba huku akiwa amelitazama jua kunaweza kufasiriwa kama njia mtoto huyo anapaswa kuandama maishani. Mtume Muhammad inasemekana ndiye wa pekee aliyesafiri juu kuzipita mbingu saba hadi akakutana na Mwenyezi Mungu. Kila mbingu aliyopitia alikutana na sampuli mbalimbali za viumbe - wazuri na waovu. Waovu waliadhibiwa na wazuri walibarikiwa. Kitendo hiki kwa hivyo kinasisitiza wosia wa mzee kuhusu maisha. Stiari ya jua ambayo vilevile inaweza vilevile kumaanisha elimu, maarifa, mwongozo wa maisha unaotoka kwa Mwenyezi Mungu. Mtume Muhammad vilevile hujulikana kama nuru kuu - yaani hekima. Mtoto huambiwa atazame jua ili akaipate hii nuru.

Mvua kwa upande ni isharaya uhai na vile vile utakaso. Mvua ndiyo ya kuziwezesha mbegu za maisha kumea na kunawiri. Mvua aidha hutakasa dhambi. Utakaso huu ni muhimu kwa maisha ya mja ya kumuwezesha kuishi maisha mema.

t^jtilca nyumba anapokaa mzazi kuna desturi inayohitaji moto kuzimwa na mwingine j^washwa tena. Hii ni ishara ya mja kutoka hatua moja ya maisha hadi nyingine.

### 3,7 Kunyolewa kwa mtoto

Desturi **hii** ya kunyolewa kwa mtoto inaonyesha mchanganyiko wa uislamu na vile vile mila za kiasili za waswahili. Isitoshe inaangazia kuhusu tofauti za kitabaka katika jamii hii ya **waswahili.** Mtoto anaweza kunyolewa baada ya siku saba au arobaine. Desturi **hii** inaweza kuandamana na Maulidi. Wale wazazi maskini wanaweza kumnyoa mtoto kwa kutumia maulidi hupitia hatua mbalimbali. Hatua ya kwanza huwa ni kumualika mwalimu mkuu wa kidini ambaye akiitikia huja kwa upande wao huhitajika wahudhurie maulidi. Ifikapo siku hiyo, waalimu huja pamoja na wanafunzi wao na vitabu vya maulidi na matari ya kuitikia vipokeo (hivi huwa ni vigoma vidogo hugongwa na kuitikia kila somo la maulidi).

Waalimu hukaa katika chumba kimoja kwenye mikeka na wanaume wengine walioalikwa. Chumba cha pili hutumiwa na wanawake na mtoto 'anayetakiwa kunyolewa. Mbele ya waalimu hawa huwa pamewekwa sinia iliyosheheni chupa ya marashi, visahani vya sukari ya mawe ya mchanga, tangawizi na vyelezo vya udi na ubani. Maulidi huanza saa nne za usiku mpaka alfajiri.

Wakati wa alfajiri mwalimu huanzisha sala. Ni wakati huu mtoto huletwa na kutiwatibu. Mtoto huyu huwa ameshikwa mikononi mama na baba au mwalimu. Tibu hapakwa juu kichwa na shingo yake. Hatimaye babake mtoto na jamaa hujitokeza na kuwapa walimu zawadi. Tibu iliyobakia hupakwa mikononi mwa jamaa waliohudhuria sherehe hiyo. Kasha

watu hao humwagiwa marashi pamoja na udi. Nyimbo huimbwa kwa wakati huu wote. Baada ya nyimbo, maulidi hukamilika, watu huenda msikitini kusali. Baada ya kusali watu hurudi na kula vyakula vilivyoandaliwa na wanawake kasha huagana na kuomba Mungu amkuze mtoto.

### 3.8 Mtoto kupewa jina

Watoto wakiwa wadogo huwa hawana majina halisi. Watoto hupewa majina ya utani kama vile panya, buku, mashavu, sanura, kifimbo, kinyerere, kidagaa, mapengo, tukwa, kibarabara, babu. Watoto wote yaani wa kiume na wa kike hupewa majina haya. Tunaona ya kwamba hakuna njia moja maalumu ya kuwapa watoto hawa majina. Watoto wanaweza kupewa majina baada ya siku saba za kuzaliwa au baada ya arobaine au baada ya mwaka. Majina halisi ya watoto yanaweza kutokana na wagomba wakiwa ni watoto wa kiume au shangazi wakiwa ni watoto wa kike.

Aidha watoto huweza kupewa majina kutokana na hali au mazingira kwa mfano mtoto anaweza kuitwa mtoro baada ya siku saba za kuzaliwa. Sababu ya kuitwa jina hili inatokana na mama kuwapoteza watoto wake wawili wanapofariki kisha wa tatu akaitwa mtoro. Mtoto wa aina hii hufungwa kamba shingoni wengine waliomtangulia. Mtoto hukaa na jina hili hadi kifo chake lakini iwapo anataka kutawala kama jumbe hutwaa lile jina alilotawala baba yake.

Hatua ya kumpatia mtoto jina ni muhimu sana kwa sababu ndiyo humpa mtoto utumbulisho katika jamii yake. Majina anayopewa mtoto yana maana fulani.

### 3 9 Mtoto kuota meno

\ltoto akiwa karibu ya kuota meno hufanyiwa dawa. Maana yake ni kuyafiinga meno ili **yasiote** vibaya yaani yasitangulie meno ya juu. Dawa ya fungo hutengenezwa na wazee kwa joichimba mizizi ya ndago. Aidha mtoto hutungiwa hirizi ambayo huivaa shingoni ili kuwezesha meno kuota. Meno yakikawia kuota, mtoto huyu hutibiwa na waganga kwa kupewa dawa inayoitwa jimbo ambayo hupakwa na kuogeshwa. Aidha mtoto hupakwa dawa ya hoza inayotengenezwa kutoka kwa majani ya miti. Muda si muda meno huanza kuchipuza.

Na iwapo mtoto atatangulia kuota meno ya juu basi hiyo hufasiriwa kama ni mkasa wa aina fulani. Zamani mtoto wa aina hiyo alikuwa halelewi na wazazi wake na hata sasa baadhi ya wazazi huwa hawampendi mtoto huyo. Wazazi humlea tu shingo upande kwa sababu ni damu yao. Mtoto huyu huwatisha watu wengine kiasi cha kutoweza kumsalimia kwa kuhofia kuambukizwa ugonjwa au kufa. Mtoto wa aina hii huitwa **kibi.**

Dhana ya kibi inawarejelea watoto wote ambao hawazaliwi katika njia ya kawaida. Watoto wa aina hii huhusishwa na mikosi. Mathalani, **kibi** vilevile anaweza kuwa yule mtoto ambaye wakati wa kuzaliwa hutanguliza kutoa miguu mbele. Huyu **kibi** ama anaweza kuuliwa au apelekwe msikini na kuwachwa huko. Watu wanokuja kusali alfajiri wakimwona hujua ya kwamba mtoto huyo amezaliwa vibaya. Hutokea mtu akamchukua na kumfanya mwanawe kisha akamtea. sababu ya wazazi wake kukataa kumtea ni kuhofia kifo.

## 10 Malezi ya mtoto

j^alezi ni sehemu muhimu sana ya kukua kwa mtoto ili kumuwezesha kuyatekeleza jnajukumu ya kijamii vizuri. Mtoto asipolewa vizuri hushindwa kuyatekeleza majukumu haya Kutofanikiwa kwa mtoto huwa ni pigo kubwa kwa familia na jamii. Familia na jamii hufedheka na hata kulaumiwa kwa kushindwa kutekeleza wajibu wake. Mtoto aliyekosa malezi mazuri huwa ni mzigo kwa jamii yake. Malezi ni asasi kubwa inayohusisha asasi zingine ndogo kama vile: ndishe na afya, usafi, nidhamu na adabu na elimu.

## 3.11 Ndishe na afya ya mtoto

Mtoto hupewa vyakula ambavyo vitasaidia katika ujenzi wa mwili wake. Kwa mfano mtoto hupewa uji wa mtama. Mtoto hupewa uji akiwa amepakatwa na mamake. Mama hutia uji kwenye kiganja chake kisha akakitumia kidole chake kumrambisha uji. Akisha kunywa uji, mama huweza kumnywesha maji au kumnyonyesha. ,Chakula licha ya kumsaidia mtoto kuimarika kiafya, humsaidia kupata usingizi.

Baada ya kuamka mtoto huoshwa uso wake na kupakwa wanja. Kabla ya kulala mtoto hunyweshwa muru na mwingine akapakwa mwili mzima. Muru husaidia katika kutuliza chango.

## 3.12 Kinga na ulinzi wa watoto

^toto huhitaji ulinzi na utunzaji wa hali ya juu. Hii inatokana na hali yake dhaifu. Mtoto **huhitaji** kinga kutokana na magonjwa, pepo na maovu mbalimbali. Kinga hufanyika kwa njia mbalimbali. Mosi kwa kuombewa. Pili, kunyweshwa na kupakwa dawa. Tatu kupungwa pepo au kwa kufungiwa hirisi za aina mbalimbali. Kwa mfano, mtoto akiwa amelala huwekewa kisu chini ya mchango. Miguu na mikono yake hufungiwa Mvunje ili kumkinga kutokana kuvamiwa na dege.

Aidha nyumba anamokaa mtoto huhitaji ulinzi ili mtoto asiweze kupata madhara yeyote. Kaa hutundikwa kwenye paa la nyumba alimolala mtoto. Kumzuia vilevile asikumbwe na dege. Asili ya ulinzi huu inatokana na imani kwamba ndege mkubwa hupita usiku kwa kila nyumba yenye mtoto na kukunjua na kukung'uta mabawa yake. Mtoto akisikia sauti ya mabawa, ijapokuwa amelala, atashtuka, asubuhi yake atashikwa na homa. Sharti apatikane mtu anayeifahamu ili amtibu mtoto.

Isitoshe mtoto, vilevile huhitaji kulindwa kutokana na watu waovu. Kama vile wachawi au wale waliojihusisha katika vitendo vya kingono. Watu wa aina hii wanapomshika mtoto bila kinga, mto hunyong'onyea mwili na hata akawa bila kinga, mtoto hunyong'onyea mwili na hata akawa dhaifu kabisa. Mtoto anaweza kuepushiwa hali hii kwa kuogeshwa maji yaliyo na **jimbo.**

### 3.13 Malezi ya watoto wenye mikosi

Tayari tumeshataja ya kwamba familia na jamii kwa jumla hufurahia ikiwa watoto watazaliwa kwa njia ya kawaida kwa mujibu wa kanuni na itikadi za jamii ya waswahili. Watoto waliozaliwa vibaya au walio na ulemavu wa aina fulani hawafurahiwi na wazazi wao kwa sababu walichukuliwa kuashiria mikosi mbalimbali. Ama watoto hawa walitupwa na wazazi wao au walilelewa shingo upande. Watoto wa aina hii waliitwa kibi. Watoto waliotupwa waliookotwa na kuletwa na watu wengine kana kwamba walikuwa wao. Watoto wengine wenye mikosi walikuwa mayatima na mazeruzeru.

Mayatima walilelewa na wanawake wengine. Watoto mazeruzeru waliashiria mkosi. Inaaminika ya kwamba watoto hawa walibadilishwa rangi yao na shetani wakati mama alipmuwacha mtoto pekee yake siku saba za kwanza baada ya kuzaliwa na kwenda chooni bila ya kinga yeyote. Chini ya mto wa kulaliwa mtoto hapakuwekwa koja au kisu wala mkononi mwake hakufiingwa mvuje na hapo ndipo shetani alipobadilisha mtoto wa binadamu, akamchukua na mahali pake akawacha wa shetani.

Aidha inaaminika ya kwamba mama wa zeruzeru alipokuwa na mimba, aliinamiwa na shetani, ndipo akazaa mtoto mweupe. Hii ndiyo maana watoto hufungwa mvuje mkononi. Mvuje una harufu mbaya asiyopenda shetani.

### 3.14 Elimu ya watoto

Elimu ni muhimu kwa mtoto kwa sababu humuwezesha kuifahamu jamii yake sawa sawa na hivyo kumsaidia kuwa mshirika kamili katika shughuli za jamii hiyo. Elimu huendelezwa katika njia mbalimbali kupitia dini na vile vile kupitia mafiinzo ya wazazi kuhusu mila na

utamaduni. Elimu hufundisha maisha kwa jumla. Hata hivyo mambo yanayotiliwa mkazo ni kama vile: Adabu, kazi mbalimbali za kijamii, majukumu ya kijamii kama vile - uzazi, ulezi, ndoa. Elimu huwahusisha watoto wote yaani wasichana na wavulana.(to be continued)

### 3.15 Elimu ya chuoni au kiislamu

**Lengo** la elimu hii ni kumfundisha mtoto namna ya kusoma na kukariri vifungu mbalimbali vya korani. Mbali na hayo, **mtoto** hufundishwa kuandika herufi za bujadi. Walimu huwafundisha watoto kuhusu kazi mbalimbali. Kazi hizi huwa zile ambazo zinategemewa sana na jamii hiyo. Ufanisi wa mja katika kazi hizi hutegemea sana imani yake ya kidini. Mja humuomba Mungu kabla ya kutenda kazi yeyote kwa mfano, mtu akianza kufyeka mwitu ili kujitayarisha kwa shughuli za kilimo, atamuomba Mungu ampe uzima na nguvu za kufanya kazi hiyo. Umuhimu wa imani husisitiziwa watoto wanapokuwa chuoni. Baadhi ya kazi zinazofundishwa ni kama vile:

(i) Kilimo - namna ya kuandaa shamba, aina'za mimea, upanzi wa mimea hiyo, matumizi yake. Mfano ni matumizi ya minazi katika jamii ya waswahili.

(ii) Biashara - aina za biashara na namna ya kutunza biashara hiyo.

(iii) Usafiri - aina za usafiri, vyombo vya usafiri, dira na namna ya kusafiri.

(iv) Uvuvi - aina za uvuvi, namna ya kuvua au mbinu za kuvua, vifaa vya uvuvi.

(v) Uundaji wa vyombo mbalimbali.

(vi) Ususu - ususi wa nywele, mikeka.

Kazi hizi hufundiswha katika misingi ya kijinsia stadi kuu zinazofundishwa ni: kuandika, jcusoma, kufikiria na kuzungumza. Hoja hii imesisitizwa na Muhammad S. Farsy (1960: 10-11).

> "... watoto hao walitiwa chuoni kusoma kuraani, dini kuandika na mambo mengine. Walipelekwa chuoni kwa ada ya kauto rupia nne, rupia mbili ni ufito wa kila mtoto. Walipofika ***Lam Yakuni*** Walipeleka mizigo ya kuni; walipofika ***Iqra Biismi*** walipelekwa bisi na walipofika ***Wassami ldhati - Lburuji,*** walipeleka kango na uji. Alimuradi ada zote za chuo wakizifuata na kuzitekeleza; wakisaidia katika kuteka maji, kuokota kuni, kufua na kupika. ... kisomo na sira waliopata chuoni uliwasaidia sana ukubwani mwao..."

dondoo hili linatudokezea kuwa elimu watoto walipata ilifuata mpangilio maalumu. Mfumo wa elimu uligawika katika viwango mbalimbali ambavyo mtoto alistahili kupitia kabla ya kuhitimu. Kila kiwango kilikuwa na mahitaji na mafunzo yake maalumu. Mfumo huu ulianzia katika usahili na kumalizikia katika uchangamano. Mfumo ulianza kwa kumfunza mtoto mambo ya kimsingi aliyoyahitaji maishani mwake. Ufanisi wa elimu ulimtegemea sana mwalimu ambaye alistahili kustahiwa. Ada ya masomo ililipwa ili kusaidia kufanikisha masomo hayo. Jambo la kusisitizwa hapa ni kwamba elimu iliyofndishwa iliwafiki sana mahitaji ya wanafunzi na vilevile ilirejelea mazingira walioyafahamu jambo lililofanya elimu yenyewe kuweza kueleweka kwa urahisi. Mwalimu alitekeleza majukumu mbalimbali: kufundisha maarifa na vilevile adabu. Alikuwa na mamlaka ya kuwarudi

watoto watundu. Mwalimu asiyewarudi watoto wanaposa adabu hukosa heshima katika jamii.

Mwalimu huweza kuwarudi watoto kwa njia zifuatazo. Kwanza kwa kumnyima ruhusa ya kwenda nyumbani na wenzake wengine baada ya masomo kumalizika. Mtoto huyu huletewa chakula chuoni na wazazi wake. Pili huweza kupigwa ka henzirani. Tatu, hukalishwa kitako huku akiwa amenyosha miguu yake iliyofungwa kamba pamoja na mikono. Nne, na mtoto huyo akiendelea na utundu wake hufungwa gogo mguuni na kipande cha mnyororo. Mtoto huyo hukaa na gogo hilo kwa siku mbili au tatu hadi aje rafiki ya mwalimu kumwombea msamaha yule mtoto.

Baadhi ya makosa ambayo yanaweza kuadhibiwa ni kama vile: kuchelewa kufika shuleni, ugomvi na kupigana au anapofanya makosa nje ya chuo, mtoto huyo anaweza kuadhibiwa kufuatia ripoti mwalimu hupokea masomo huanza asubuhi mwendo wa saa kumi na mbili hivi na kukamilika saa kumi za jioni.

### 3.16 Elimu nje ya chuo

Elimu inaendeshwa nyumbani na wazazi au katika asasi muhimu ya tohara. Mtoto akifikia umri wa miaka sita au saba hufundishwa sana mambo yanayohusiana na adabu. Mtoto hutarajiwa sana kusikiliza amri ya wazee wake. Iwapo wamemkataza neno, lazima asikilize. Mtoto hufundishwa kuwaamkia watu hasa wakubwa wake, aidha hufundishwa kuwasogelea watu wazima asikae kabla ya wao kukaa. Na iwapo amekaa mbele ya watu wazima

hatarajiwi kubwabwaja maneno ovyo ovyo wajibu wake ni kusikiliza amri atakazopewa na wakubwa wake. Mtoto anaweza tu kuzungumza na kucheka ikiwa amekaa na vijana wenzake. Iwapo mtoto amefuatana na babake au mwalimu wake, haruhusiwi kumtangulia mbele. Kufanya hivyo ni utovu mkubwa wa adabu.

Kadhalika mtoto haruhusiwi kutoa hadharani aibu za watu. Mathalani, kuzungumzia habari ya mke wa fulani hupika chakula kibichi, au leo fulani wamelala njaa, nyumba yao ni giza totoro haina taa. Hii ndiyo maana mara nyingi wazee huwakataza watoto wao kuficha siri.

Na iwapo wegeni wamekuja nyumbani mtoto haruhusiwi kunawa mikono kabla ya wageni wakati wa kula. Na ikiwa hapana mtu mwingine katika nyumba hiyo wa kuwanawisha wangeni basi, mtoto huchukua jukumu hilo. Wakati wa kula, iwapo mlo huo unahusisha kitoweo cha nyama haruhusiwi kuokota vipande vya nyama na kuvitumbukiza kinywanni bila kupewa idhini na wakubwa wake. Isitoshe wakati huo wa kula, mtoto haruhusiwi kutafimatafuna chakula mithili ya mbwa. Tabia hii hu'ashiria ulafi. Aidha ni mwiko kwa mtoto kwenda miayo hadharani. Tabia hii inawenaweza kufasiriwa na watu kuwa ni uhaba wa chakula au mtoto huyu hatunzwi vizuri. Mtoto akienda miayo hukaripiwa kwa kuambiwa ya kwamba akifumbe kinywa wakati wa kwenda miayo, asikiwache wazi kama kinywa cha mammmmba. Kinyua chake hulingaishwa na cha mamba kwa sababu mamba akiwa na njaa, hukaa juu ya ukingo wa mto akaacha kinywa chake wazi nzi waingie ndani ya kinywa; kisha hukifumba kinywa hicho.

Mambo mengine ambayo hayaruhusiwi ni kama vile kwenda mbweu na kwenda chafya wakati wa kula. Kila mtoto sharti asikilize amri za watu watatu iwapo anataka radhi za mungu. Amri ya kwanza ni ya mfalme, pili ni ya wazeee wake na ya tatu ni ya mwalimu. Desturi zilizotajwa hapo juu mbali na kumtukuza mtoto akiwa na maadili mema, vilevile zilinuiwa kumwepusha na mikisi-kama vile ya kusakamwa na chakula kuoni au kuingiwa kinywani kwa vitu hatari wakati wa kwenda miayo.

### 3.17 Tohara

Tayari tumeshataja kuwa kuzaliwa kwa mtoto huambatana na sherehe ya kumkaribisha kujiunga na jumuia ya binadamu. Hata hivyo mtoto huyu sharti aandaliwe barabara ilk aweze kufikia kiwango cha kutegemewa au kuwa mshirika kamilii wa shughuli. Anapofikia umri fulani hutarajiwa kuvuka mpaka ya utoto na kujiunga na utu-uzina kimaumbile au kumbo na hali kadhalika kijamii na kidino.Tohara huwa aabasi muhimu inayomuwezesha kijana kukaribishwa katika utu-uzima. Huweza kulinganishwa na mtihani fulani kijana anasatahili kupia.

Tohara katika jamii nyingi za Kiafrika anavyosema J.S Mbiti (1969:121-2) inaweza kufasiriwa katika njia nyingi.Kwanza, tohara humpa barubaru fursa ya kufundishwa kuhusu maisha ya kujumuia na kijima ya jamii yake. Jambo hili hufanyika pale barubaru anapoigura familia yake kwa muda hadi msituni au kumbini. Wakati huu wakiwa kumbini, mabarbaru hupata mafunzo mbalimbali kutoka kwa makungwi au manyakanga wao.

Mafunzo yanahusu maisha kwa jumla. Baada ya mafunzo haya; vijana hurejea makwao. Kitendo cha kugura na kurejea nyumbani kinaweza kumithilishwa na kufa na kufufuka kwa mja. Kurudi nyumbani baada ya mafunzo kunaashiria kuzaliwa upya kwa kijana. Yaani Barubaru ashaupita mtihani wake sasa ni mtu mzima. Kupita kwa mtihani huu humpa ruhusa ya kutekeleza majukumu ya kiutu - uzima kama vile kuoa, kujihusisha katika ngono, na kuzaa ili kukiendeleza kizazi na jamii kwa jumla. Tohara kwa hivyo ina umuhimu mkubwa. Humwezesha kijana kupata maarifa, aidha kujifunza kuhusu uvumilivu, namna ya kuishi na watu wengine, kutii amri. Isitoshe hujifunza kuhusu siri zinazozunguka uume na uke.

Sherehe ya tohara ni muhimu kiasi kwamba yeyote asiyeipitia hata akiwa na umri mkubwa ulioje bado angali anachukuliwa kama mtu mchafu. Hali hii humnyima fursa ya kutekeleza majukumuu ya kijamii kama vile - kutoa nasaha na katika jamii nyingine huenda asiruhusiwe kuuoa.

Tohara katika jamii hii ya waswahili wa mrima huhdsiaha wavulana na wasichana baina ya miaka 9-14. Hata hivyo kuna wale wanaotahiriwa wakiwa na miaka mitano hadi saba.

### 3.18 Tohara ya mtoto wa kiume.

Mtoto akifikisha umri wa kutahiriwa hupelekwa kumbini. Kabla ya kupelekwa kumbini, badaaye mtoto hualika jamaa zake mkesha wa kutahiriwa na kucheza manyago (ngoma inayochezwa wakati wa tohara). Alasiri hiyo baba na jamaa zake mtoto huandamana hadi makaburini kufanya makafara. Lengo huwa katika radhi za wafu ili kuifanikisha tohara. Watu hawa hufagia kaburi, huyang'oa majani yaliyomea karibu na kaburi hilo kasha

wakazizoa taka zote zilizopo. Harafu ubani hutiwa ndani ya chetezo na kuwekwa chini ya kichwa cha kaburi. Kuchomwa kwa ubani huwa njia ya kuomba rehema za mwenyezi Mungu na vilevile hufukuza mbali mkosi wa aina yeyote ile.

Ifikapo usiku, jamaa zake mtoto pamoja na watu wengine hukusanyika kucheza many ago. Asili ngoma hii kuitwa manyago ni kwamba wakati wa alfajiri hufanyika vituko vya kila aina. Kwa mfano kutengenezwa miti iliyofungwa majani kasha mtu akaingia ndani kucheza. Mtu huyu huwa na miondoko ya jinyama Fulani kama vile ngamia, tembo au mbwa. Chakula na tembo huandaliwa wakati wa kucheza manyago. Ngiriba au Mwinzi huwepo na hata yeye hushiriki katika uchezaji wa manyago. Ngariba huwaalika Ngariba wenzake kushiriki katika namna ya manyago.

Inapowandia alfajiri wakati wa manyago yanapovunjika, ngariba huingia ndani ya banda lililojengwa watoto wanatoka kutahiriwa. Watoto hawa hawaruhusiwi kushiriki katika manyago. Banda hilo ndilo huitwa **kumbi** au **jando**/kwa sababu ndilo hutumika kuwaficha watoto na huwa limenjengwa mwituni. Wanawake na wanaume wasiotahiriwa hawaruhusiwi kiungia kumbini. Ngariba anapoingia kumbini huwa yuko tayari kufanya kazi yake ya kutahiri. Huwa amekibeba kijemne kinacho julikana kama **kirimbo.** Akifika humwita mwari mmoja. Huyu mwari wa kwanza hujulikana kama **kiranja.** Mara nyingi kiranja huwa mtumwa. Kiranja huwekwa juu ya **tego,** yaani kibao cha kukaa mtu mmoja tu. Kiranja hushikiliwa na mtu ambaye huitwa shuwalLmsaidizi wa Ngariba, na hapo Ngariba humtahiri yule mtoto kwa kile kijembe.

tfuu huwa mtihani mgumu unaohitaji uvumilivu mwingi. Baadhi ya wanaotahiriwa hushindwa kuvumilia na wengine wakiwaona wenzao wakilia kwa uchungu hutaka kulivunja franda hata watoroke. Baada ya kutahiriwa kila mtoto hutiwa dawa. Kazi ya kumuuguza mwari hufanywa na kungwi. Kila mwari huwa na kungwi wake. Kila asubuhi huja kungwi na kumwitia mwari dawa Baada ya siku sita, watoto waliotahiriwa huitwa katika sherehe inayoitwa **mogo** Mogo huwa ni kuoga kwanza mwari hufanya baada ya kutahiriwa. Wanaweza kupelekwa katika mto uliopo karibu au wakiwa karibu na bahari basi watapelekwa huko. Watoto hawa hupakwa dawa maalumu baada ya kuoga. Kisha hurejea tena kumbini. Jioni wazazi wao huwaletea tui pamoja na pamba, linalotumiwa na shuwali au kungwi kuwapa kwenye majeraha yao. Wakati haya yanafanyika, wimbo huwa unaibwa.

**'Nigemapo tembo moyo wanatetema'**

Shuwali au kungwi anapoimba maneno haya, wan huitikia vile vile.

Kungwi na shuwali hukaa siku zote kumbini na wale wari, lakini ngariba huyu mara moja tiuwatazama. Na anapokuja huwaamkia watoto:

**'Wari, inbukwa'**

Nao wakamjibu!

**Mbukwa ngariba***

Wale watoto hufundiswa adabu na makungwi zao, kwa mfano kuwatazama vyema wazee wao, kumchelea hakimu, kumcha mwalimu wao, kuwaheshimu wapita njia, kukaa na wake yyema majumbani. Isitoshe watoto hawa hufiradisha nyimbo na ndani ya nyimbo hizo huwa

mna mafumbo ambayo huhitaji kufumbuliwa. Wimbo ukishaimbwa mtoto huulizwa maana yake. Na asipojua hupigwa na kasha huambiwa maana yake. Hii huwa njia ya kunoa bongo za watoto ili kuwapa uwezo wa kutatulia shida mbalimbali watakazo kumbana nazo maishani. Si hayo tu, ufumbuaji wa mafumbo ni njia ya kumsaidia mtoto huyu kufasiri sawasawa mazingira yake Aidha njia ilitumiwa kupima uwezo wake wa kufikiria na aina ya maarifa aliyokuwa nayo.

Na wale watoto wanapopona, ngariba huwapelekea habari wazazi wao. Habari hii huwasaidia wazee hao kufenya maandalizi ya kuwapokea watoto wao. Watoto hawa hununuliwa nguo mpya. Watoto hucheza manyango usiku kucha karibu na kumbini. Asubuhi ifikapo, watoto hunyolewa Baba na ndugu za watoto hawa hupewa lakini hawaruhusiwi kusema chochote nao.kunyolewa kwa watoto hawa hupigwa zumari na siwa. Wakati huo huwa wamekaa juu ya vitl Wakishanyolewa watoto hawa hupelekwa vyooni kuoswa na wakirudi huvishwa mavazi yao mapya. Zile nguo zao kuukuu pamoja na mikeka waliyotumia kwa kulala hupewa makungwi wao. Tena hupelekwa mjini huku wakiimbiwa nyimbo na ngariba!

'Siwalile wana wenu, siwalile?

Watu huitika ule wimbo, wanawake hupiga vigelegeie na kumwaga mchele kuwafurahia watoto wao na wakifika nyumbani hutunzwa na kuandaliwa vyakula vitamu vitamu. Watu husherehekea kuadimisha kufuzu kwa kijana. Kucheza na kufurahia kwa pamoja hukuza umoja na mshikamano wa watu katika jamii hiyo. Kunyolewa kwa nywele na kuogeswa

huashiria utakaso unaoambatana na kufuzu kutoka utotoni hadi ukubwani. Mtoto sasa huwa amekaribishwa rasmi katika jamii, si tu wa mamake na babake mzazi bali ni mali ya jamii. Chochote anachokifanya ni kwa manufaa ya jamii.

3.19 **Tohara ya mtoto wa** kike.

Mtoto wa kike wa miaka saba huitwa kigori, hata akipata miaka kumi huwa mwari au mwanamwali. Wazazi wake wakumuona ameshavunja ungo mara moja humpelekea habari kungwi wake. Kungwi huja bila kukawia na kumchukua mwari hadi kwake kwenda kumwalika, mwari haonekani na watu wengine isipokuwa kungwi na jamaa zake. Mwari hukaa kwa kungwi kwa miezi sita au mwaka mzima Hata hivyo kuna wale ambao hukaa mwezi mmoja tu kisha wakarejea kwa wazazi wake.

Mwari akiwa kwa kungwi hufundishwa mambo mengi sana. Mwari hufundiswa kujitunza vyema na kukaa vyema na watu kuwaheshimu Aidha hufundiswa kupika na kusuka mikeka, vilevile hufundishwa namna ya kukaa na mumewe akishaolewa. Kungwi humpa mwari jiwe la msio laini lenye umbo la duara ambalo hulitumia kusagia viungo kama tibu, dalia, maua maulidi na kila aina ya manukato anayotumia kujisingia yeye mwenyewe. Jiwe hilo pia hutumika hata baada ya yeye kuolewa.

Wakati wa kukaa kwa kungwi unapomalizika, kungwi huwajulisha wazazi wake mwari anahitajika kupelekwa **Muyomboni,** aina ya mti maalumu au mahali mwari hupelekwa ili hufundiswa kuhusu ngono na mapenzi Habari hii inapowafikia wazee wa mwari, wao hutengeneza pombe na togwa. Huko muyomboni, wanawake wengi hukusanyika na wari

wengine pia. Wari hufichwa ili watu wasiwaone. Hupelekwa muyomboni usiku wakiwa wamebebwa na wanawake. Kungwi huwakika wari wake, wengine waliotangulia zamani sita au saba hivi kumpeleka mwenzao muyombini. Nao ni lazima waje kwasababu wari sharti wamtii kungwi wao.

Wakishampeleka yule mwari kumbini, humchzea ngoma ya unyango, na hapo palipo na unyango hupigwa ngoma, inayoitikiwa na wanawake na wari. Nyimbo za mizungu huimbwa. Mwari huwekewa kitu nyuma ya mgongo wak, akakitwaa kile kitu kwa mdomo akiwa amejiinamia nyuma huku akiitikia ngoma na nyimbo zinazoimbwa. Wale makungwi wakishaimba naye mwari akashindwa kung'amua maana ya wimbo fulani au akiwekewa mizungu asiweze kutwaa, mwari huyo hupigwa kabla ya kuambiwa maana yake. Aking'amua maana ya mzungu, wanawake wote humwambia kwa sauti kubwa. **Cheleko, cheleko_** maana yake, kizazi changu, kizazi changu kizuri). Na wari wasipofahamu mizungu waliowekewa huimbiwa!

**'Kazongo, he, leo Kazongo'**

Maana yake, taabu leo, taabu. Wasiojua mizungu hupigwa kisha hatimaye akaonyeshwa.

Siku ya saba wari hupelekwa muyombini. Makungwi wote na wari hukaa wakipiga ngoma na kucheza. Na pakiwa na pombe basi pombe hiyo hunywewa. Ifikapo jioni wari hunyolewa, wakichegiwa sekini usoni na kupakwa wanja. Vichwani vilivyonyolewa hupakwa dalia, kisha huviswa mavazi mapya na kupambwa vyombo vya fedha inapofika jioni wari huletwa mjini wanakokaribiswa kwa taadhima kwa kupewa kila aina ya tunu.

luwa hawana ruhusa ya kusema na mtu isipokuwa yule mtu aliyewatambua. Wari lutembezwa kwa muda wa siku tatu. Na hizo siku zinazomalizika wao huvuliwa mapambo /akapewa mavazi ya kila siku kuvaa.

Lama ilivyoelezewa katika tohara ya wavulana, lengo la tohara ya wasichana huwa uwavusha daraja na kuwaingiza katika utu uzima ambapo atatarajiwa kuihudumu jamii kwa jasiri na busara. Kule kupigwa kwa sababu ya kushindwa kung'amua mizungu au yale lafumbo yanayojitokeza katika nyimbo, hunuiwa kumuandaa kwa vizunumkuti vya maisha mbavyo huhitaji akili pevu, ubunifu subira na uvumilivu kuweza kuvitatua. Kushindwa uvitatua vizungumkuti hivi na sawa na kushindwa kuvitatua na maisha. Makosa au pungufu wa mtu mmoja unaweza kuiletea familia au jamii balaa kubwa. Kwa hivyo ni ikumu la jamii kuwaandaa watu vilivyo wasije wakakosea.

**.20 Ndoa.**

amii za Kiafrika huchukulia ndoa kama uti wa mgongo wa maisha. Ndoa ndiyo huwaletea amoja wanajamii wote: wale ambao hawajazaliwaa, walio hai na hata wafii. Baada ya )hara vijana hutarajia kuoa au kuolewa . ndoa ni mtihani mwingine unaothibitisha ukomavu /a mtu au la . ukomavu huu utathibitiswa zaidi na namna anayehusika anavyoyatekeleza lajukumu mbalimbali katika jamii, ndoa hali kadhalika ndio njia ya kupanua au kuendeleza amilia au kizazi. Jambo hili litawezekana tu kupitia kwa kuzaa watoo.

Jwezo wa kupata watoto ndiyo huimarisha ndoa na vilevile huendeleza jamii. Kupitia kwa doa wale wanaozaliwa huyajaza mapengo yaliyowachwa na wenye waliofariki. Isitoshe

wazee hupata wasaidizi kwa hivyo ndoa na uzazi huhakikisha jamii fulani haifi. Ndoa pamoja na uwezo wa kuzaa kuwapa watu staha katika jamii. Kwa hivyo kutokana na maelezo haya tunaona ya kwamba ndoa isiyoweza kubarikiwa na watoto kuchukuliwa kuwa ni mkosi kwa sio tu walioana bali kwa jamii nzima kwa jumla. Hii ndiyo sababu inayozifanya jamii nyingi hushutumu utasa na ugumba. Kwa upande mwingine, mume au mtu anayekataa kuolewa au kuooa hudharauriwa na kufanyika kila aina ya mizaha.

### 3.21 Uchumba.

Asasi ya ndoa kama ilivyoelezewa katika **Desturi za Waswahili** hupitia hatua mbalimbali. Kuna hatua ya maposa, kuchumbiana, Arusi na wakati mwingine talaka na kuachana hutokea. Katika jamii ya waswahili wa mrima, mtu akitaka kuoa kwanza huposo. Jamii yake yule mwanamke ndiye hutumwa kupeleka habari ya posa. Huyu huitwa <u>Mshenga au mjumbe.</u> Watu wengine humtuma mshenga kumsemea maneno babaye mchumba na wengine huandika barua. Wakishapatana, mposaji na mshenga, huulizwa apewe leso aandike barua. Mara yule mchumba mume hutoa leso, na mshenga huandika barua hivi

'Mvele wangu Fulani bin Fulani,

nakuarifu amekuja mtoto wa fulani, anataka binti wako kumwoa, na hayo ni mambo ya heri. Mtoto mwanamke bidhaa mbovu kama baruti na moto, au kama pamba na moto, au kama kitunguu. Tafadhali ukasoma barua, nataka majibu, nawe niwie radhi sana.

Wasalaam

Ikishakwisha ile barua, bahasha yake huwa ni ile leso maana ndiyo heshima kubwa mtu hutunukiwa. Baadaye mtu akisha soma ile barua, huwaita jamaa zake, wake kwa waume kutafuta ushauri wao. Wengine watakubalii na wengine wataka wapewe kitu kidogo na mchumba mume, naye atatoa kitu awape wale wenye ugomvi. Hapo watasema, manemo yamekwisha, huyu ndiye mume. Mshenga atamwarifu mposaji kwamba wakwewe wameridhi wote. Yule mchumba mume atanunua kila zawadi kumpelekea mchumbawe kama nguo nzuri au matunda yaliyoiva. Licha ya kubadilishana zawadi hawa wachumba hawaruhusiwi kuonana, tokea siku ya kupelekwa fedha hadi siku ya arusi.

Mshenga atarejea tena na kuuliza kiasi cha mahari wanachokitaka. Mshenga huuliza hivi: "Kiasi gani kilemba chenu na hari yenu?" Baba-mtu atajibu" Kilemba changu kiasi fulani na mahari kiasi fulani". Mshenga hurudi kwake na kumpa mchumba habari zile na akikubali na fedha anazo humpa mshenga na kuzipeleka kwa mkewe. Kama mkwewe amekufa, hupewa ndungu yake au babu yake.Kama hakuna jamaa yake yeyote basi atapewa mwanamke mwenye we.

Baba akiisha pewa hizo fedha huwaita jamaa zake kuwaonyesha na hatimaye kugawana. Fedha hizo huitwa **Kifunga mlango** au **kifunga uchumba.** Kuashiria ya kwamba sasa uchumba umekwisha. Fedha hizi hugawanywa katika mafungu mbalimbali kulingana jamaa waliopo. Fungu la kwanza **(Uweleko/ubeleko kondari)** humwendea mama, hii huwa ni ahsante au shukrani kwa kazi ya ulezi aliyoifanya. Fungu lingine humwendea shangazi wa mtoto. Mafungu mengine huwaendea jamaa wengine waliosalia.

Baada ya uposa, wakwe hutaka mahari kamili kulipwa. Baada ya sku chache yule mume humtaka mkwe. Atamwambia mshenga wake siku ya kuoa.Na ikiwa siku hiyo imekubaliwa, babaye mke atawaarifu watu waliomhusu "Siku fulani nina kikombe cha kahawa"

### 3.22 Kikombe Cha Kahawa

Hakika siku hiyo haipikwi kahawa bali vyakula vinginevyo huandaliwa. Alasiri hupigwa **tari la njia.** Hii huwa ni aina Fulani ya ngoma.Vijana wote huvaa majambia na panga mikononi na kucheza huku wanawake wamechukua maua na mashada waliyonunua kwa mapesa yao. Wanawake huwapa wanaume mashada haya wanapocheza nao hucheza polepole na wafikapo nyumbani pa harusi wanawake hupiga vigelegele. Wachezaji humwagiwa marashi wote wanawake huwapa wanaume mashada haya wanapocheza nao hucheza polepole-na wafikapo nyumbani pa harusi wanawake hupiga vigelege. Wachezaji humwagiwa marashi wote wanawake kwa wanaume; tena hupewa tabuu kutafuna. Mshenga hupewa upatu wa tambuu. Ni wakati huu watu wanapofahamishwa siku ya harusi. Siku yenyewe hutangazwa na mjumbe Fulani kwa jamaa. Huyu mjumbe hutumia 'ngoma kutangazia. Baadaye tari la kudiriji huchezwa; uchezaji wake huwa hautofautiani sana na ule wa kucheza tari.

### 3.23 Kupiga pamba na harusi

Siku nne au tano baada ya watu kunywa kikombe cha kahawa, hualikwa tena wanawake na wanaume na mshenga kwenda kupiga pamba. Baada ya siku mbili au tatu watu wale huarifiwa tena na mshenga, naye mwenyewe huenda kila nyumba kuwaarifu kina mwana na kina bwana, kuwa wanaalikwa kwa babaye harusi kushona godoro na mto. Mafundi huitwa

Baada ya uposa, wakwe hutaka mahari kamili kulipwa. Baada ya sku chache yule mume humtaka mkwe. Atamwambia mshenga wake siku ya kuoa.Na ikiwa siku hiyo imekubaliwa, babaye mke atawaarifu watu waliomhusu "Siku fulani nina kikombe cha kahawa"

### 3.22 Kikombe Cha Kahawa

Hakika siku hiyo haipikwi kahawa bali vyakula vinginevyo huandaliwa. Alasiri hupigwa **tari la njia.** Hii huwa ni aina Fulani ya ngoma.Vijana wote huvaa majambia na panga mikononi na kucheza huku wanawake wamechukua maua na mashada waliyonunua kwa mapesa yao. Wanawake huwapa wanaume mashada haya wanapocheza nao hucheza polepole na wafikapo nyumbani pa harusi wanawake hupiga vigelegele. Wachezaji humwagiwa marashi wote wanawake huwapa wanaume mashada haya wanapocheza nao hucheza polepole-na wafikapo nyumbani pa harusi wanawake hupiga vigelege. Wachezaji humwagiwa marashi wote wanawake kwa wanaume; tena hupewa tabuu kutafuna. Mshenga hupewa upatu wa tambuu. Ni wakati huu watu wanapofahamishwa siku ya harusi. Siku yenyewe hutangazwa na mjumbe Fulani kwa jamaa. Huyu mjumbe hutumia ngoma kutangazia. Baadaye tari la kudiriji huchezwa; uchezaji wake huwa hautofautiani sana na ule wa kucheza tari.

### 3.23 Kupiga pamba na harusi

Siku nne au tano baada ya watu kunywa kikombe cha kahawa, huaiikwa tena wanawake na wanaume na mshenga kwenda kupiga pamba. Baada ya siku mbili au tatu watu wale huarifiwa tena na mshenga, naye mwenyewe huenda kila nyumba kuwaarifu kina mwana na kina bwana, kuwa wanaalikwa kwa babaye harusi kushona godoro na mto. Mafundi huitwa

kulishona hilo godoro wakisaidiwa na watu wengine kutia pamba katika mifuko. Baadaye lile godoro na mito mitatu hupelekwa katika chumba cha Bi. Harusi na kufunikwa nguo.

Harusi hufanyika katika nyumba ya wazee wa harusi mwanamke. Asubuhi ya harusi nyumba hupambwa, vizuri na kila sehemu ikanadhifiwa vizuri. Alasiri huja shogaze bi arusi kumpleka chooni kumwosha na kumpamba. Baadaye huja kungwi kisha wakaamkuana na Bi Harusi. Baada ya kulipa ada zinazohitajika, mume huenda ukumbini. Nyimbo na ngoma mbalimbali huandamana na sherehe hii. Baada ya shughuli zote. Bwana na Bi Harusi huonana kisha ikafuata fungate.

### 3.24 Elementi za mwonoulimwengu katika desturi za waswahili

Baada ya kuziangalia hatua mbalimbali za maisha ya waswahili, kazi hii vilevile itaangazia elementi za mwonoulimwengu zinazojitokeza katika **Desturi za Waswahili.** Baadhi ya elementi zinazojitokeza ni kama vile: -

(i) Kinga dhidi ya hatari.

(ii) Nguvu ya sala.

(iii) Matumizi ya uwezo na madaraka.

(iv) Ujumi

(v) Ujamaa na uendelezaji wa kizazi.

(vi) Usambazaji na uhifadhi wa maarifa.

(vii) Usababishi wa misukosuko.

(viii) Utakaso.

(ix) Afya bora.

(x) Ushujaa na uvumilivu.

(xi) Ujamaa na mshikamano wa jamii.

### 3.25 Kinga dhidi ya hatari

Jamii ya waswahili hutambua kutokea kwa hatari mbalimbali. Kuna hatari inaaminika zinaweza kusababishwa na mazingira wamamoishi majini, mashetani na pepo. Hatari hizi zisipokingwa huweza kusababisha madhara kama vile magonjwa, ulemavu au vifo. Naye mtoto aliyezaliwa hurembwa wanja katika vyungo vyake vya mwili. Aidha hufungwa mivunje na vigwe. Lengo la haya yote ni kumkinga mtoto huyo dhidi ya hatari yeyote hasa pepo. Isitoshe wasichana na wavulana wanapokuwa wanatoka kumbini na kuelekea mjini, hufunikwa gubigubi ili wasiweze kuonekana hadharani. Hii ni kuwakinga dhidi ya uovu wowote unaokuwa umelengwa kwao. Mara kwa mara sala na makafara hufanywa ili kuikinga jamii kutokana na hatari.

### 3.26 Nguvu ya sala

Sala ina umuhimu mkubwa katika maisha ya waswahili. Nguvu zake zimetanda katika kila kipengee cha maisha yao. Sala inategemewa kutoa suluhisho kwa kila shida au vizuizi vya jamii hiyo. Kwa mfano sala inaweza kutegemewa kumbadilisha mtoto mtundu au kumuwezesha mtoto kupata maarifa hata akawa muungwana. Aidha sala humsaidia mama kujifungua salama salimini - watu humzunguka mama huyo wakati akipiga kite cha uzazi, wakamwombea hatimaye kujifungua mtoto asiye na dosari.

Sala hutegemewa kufanikisha tohara, malezi, uchumba, arusi, kazi mbalimbali - biashara, uvuvi, ubaharia, kilimo, usanaji wa vyombo mbalimbali na uwindaji. Sala hutegemewa katika safari. Chochote kinachofanywa bila ya sala hakitarajiwi kufanikiwa. Sala haitegemewi tu katika kuepusha balaa bali hutegemewa kudumisha ufanisi. Kila ufanisi wa aina yeyote ukipatikana, sala ya kumshukuru Mungu hutolewa. Sababu kuu ya kufanya hivyo huwa kumuomba Mungu aendeleze ufanisi huo. Sala hutegemewa kuwapa watu moyo wa kuwaliwaza.

### 3.27 Usambazaji na uhifadhi wa maarifa

Ukuaji wa jamii hutegemea mfumo wake wa maarifa. Maarifa haya yanaweza kuhifadhiwa na kusambazwa kwa njia maalumu zilizokubaliwa na jamii hiyo. Jamii hutegemea asasi mbalimbali kufanikisha lengo hili. Asasi hizi ni kama vile shule, dini, tohara na ndoa. Jamii ya Waswahili ilitambua umuhimu wa maarifa. Lengo kuu la usambazaji wa maarifa lilikuwa kujenga jamii yenye watu waadilifu, wenye akili tambuzi na bunifu; kuhifadhi mila za jamii ili kuwawezesha watu kutosahau asili yao. Aidha'elimu ilifundisha maarifa ya kikazi, unyumba, na maarifa kuhusu majukumu mbalimbali ya kijamii na elimu ya ngono.

Maarifa haya yalisambazwa misikitini, madarasani, manyumbani, kumbini (jandoni) na hata muyomboni. Wajuzi mbalimbali walihusika katika kuyasambaza hayo maarifa. Hawa wajuzi walikuwa: wazazi, walimu wa kidini, manyakanga au makungwi, wazee mbalimbali, ngariba, wasanii mbalimbali, wachezaji ngoma, waimbaji, wafumbaji wa mafumbo. Wote hawa walichangia sana kuyapevusha mawazo ya wanafunzi. Wanafunzi (wanafunzi

madarasani, wari na wanagenzi) walitarajiwa kupita mitihani. Waliofeli waliadhibiwa kabla ya kuambiwa majibu. Waliofaulu walituzwa na kushangiliwa.

### 3.28 Afya bora

Uthabiti wa jamii hutegemea sana siha ya watu wake. Waswahili walitambua hili kupitia njia zifuatazo: Mosi walipendekeza ndishe bora kwa mama wajawazito, mama waliojifungua na watoto waliozaliwa kwa kupewa vyakula vilivyojenga mili yao. Aidha jamii hii ilipambana na magonjwa mbalimbali yaliyowahijumu wanajamii. Wawele walikwenda kwa waganga kutibiwa.

### 3.29 Ushujaa na uvumilivu

Hizi zilikuwa mojawapo ya elementi muhimu za mwonoulimwengu wa waswahili. Maisha ni mkururo wa mitihani na vizingiti mbalimbali vinavyohitaji ushujaa na uvumilivu. Mikasa ya shida zilizotokea kwa mfano magonjwa, vifo, mikasa ya kimaumbile, ulemavu zilihitaji uvumilivu na ujasiri kukabiliana nazo. Asasi mbalimbali za kijamii kama vile tohara, dindi, uzazi. Ziliwaandaa waja kukabiliana na matatizo haya. Asasi hizi zilifundisha uvumilivu wa moyo, na wa mwili, ushujaa na uthabiti wa moyo.

### 3.30 Ujamaa na mshikamano wa jamii

Maendeleo ya jamii yalitegemea sana mahusiano yake. Maisha ya waswahili yalikuwa ya kutegemeana kwa watu. Lengo kuu lilikuwa kudumisha utu. Mtu alisemekana kuwa muungwana au mstaarabu ikiwa vitendo vyake vilijuwa vimemfikisha daraja ya juu ya utu. Utu ndiyo uliojenga msingi madhubuti wa mshikamano wa jamii. Hatua mbalimbali za

maisha ziliwatangamanisha watu - iwe wakati mtoto amezaliwa, wakati wa tohara, wakati wa ndoa, wakati wa kusali, wakati wa matambiko. Msiba wa mtu mmoja ulioombolezwa na kila mtu. Sherehe zozote kama vile maulidi zilihusisha kila mwanjamii. Na isitoshe ujamaa huu uliendelezwa kupitia kwa ndoa. Ndoa ilileta pamoja familia mbalimbali.

### 3.31 Ujumi na utakaso

Sherehe zinazoambatana na hatua mbalimbali ni matukio ya kiujumi. Sherehe ziliwapa waswahili fursa ya kuelezea au kudhihirisha hisia zao. Tayari imeshatajwa katika kazi hii kuwa kila hatua ya maisha ya waswahili iliambatana na sherehe maalumu. Sherehe hizi zilihusisha na nyimbo, mashairi, ulumbi, malumbano ya kiutani, kufumba na kufumbua mafumbo, viapo. Wahusika walivaa mavazi rasmi (maleba) yaliyoafiki sherehe hiyo. Baadhi ya mavazi haya yalikuwa ya kiufundi sana. Ujumi ilikuwa zao la jamii maana sherehe hizi ziliwahusisha takribani watu wote.

Utakaso vilevile lilikuwa tukio la kiujumi. Usafi ,wa kila kitu ulikuwa lengo la kila mwanajamii. Usafi wa vitendo, na usafi wa roho ulisisitizwa. Chochote kibaya kilichofanyika kilitia ndoa usafi wa jamii. Hii ilikuwa pamoja na kukiuka mila za jamii. Matambiko na sala yalitumiwa kutakasa jamii kutokana na najisi iliotiwa jamii hiyo. Tohara ya watoto vilevile lilikuwa tukio la utakaso yaani kuondolea jamii uchafu na kuupa upya tena yaanni 'kuizaa' jamii upya.

### 3.32 Uyakinifu wa mwonoulimwengu wa Waswahili

Tayari imetajwa katika kazi hii ya kwamba hatua mbalimbali za maisha walizopitia waswahili ni matukio ya kihalisi. Watoto wanazaliwa, wanapewa majina, watoto wanaugua, wanatibiwa, watoto wanalelewa, wanapashwa tohara, wanaoa na kuolewa, na wanafariki. Aidha katika utu uzima wao walijifunza na kufanya kazi ili kutimiza mahitaji yao.

Chochote kinachofanyika katika maisha ya waswahili kina uamilifu na maana. Maana hii iliweza kueleweka barabara na waswahili wenyewe kwa sababu shughuli zote za kijamii huwahusisha watu wote. Kwa hivyo sherehe zao, ngoma, nyimbo, viapo, sala, matambiko, maigizo yao na kwa jumla desturi zao ni mambo yaliyo halisi. Itikadi kuhusu pepo, mashetani, uchawi na kupungwa kwa pepo ni mambo yalikuwa halisi katika mwonoulimwengu wao. Tunahitimisha seheme hii kwa kusema kwamba, madamu kila kituna kila tukio, lina maana na uamilifu katika jamii basi vitu hivyo na matukio hayo ni halisi au yakinifu.

*i*

### 3.33 Hitimisho

Sura hii imeangazia hatua mbalimbali za maisha kuanzia kwa kuzaliwa hadi wakati wa kuona. Hatua hizi ni sehemu muhimu hadi wakati wa kuoana. Hatua hizi ni sehemu muhimu ya mwanaulimwengu wa waswahili. Na kama inavyobainika kila hatua ni muhimu katika maisha ya waswahili. Umuhimu unathibitisha na sherehe zilizoambatana na kila hatua ya maisha.

# SURA YA NNE

## 4.0 Hitimisho

Hii ni sura ya kuhitimisha tasnifu. Mambo kadhaa yanajitokeza. Kila jamii ina mwonoulimwengu wake.Ubora na uchangamano wa mwonoulimwengu fulani ni masuala ya mjadala ambayo hayana jawabu moja. Jambo linalojitokeza hapa ni kwamba wale wale wahusika na washiriki katika utamaduni ndiyo waliyo katika nafasi ya kuuelewa utamaduni. Wataelewa na kufasiri sawasawa misimbo ya utamaduni, watazielewa falsafa na mifumo ya utamaduni, watazielewa falsafa na mifumo ya maisha ya jamii husika. Ni muhimu ikumbukwe hapa kwamba utamaduni huhusisha uhusika na wal siyo utazamaji au **"ushabiki",** Ni tukio la kihisia na kifikia.Hakuna utamaduni ambao unaweza kudai hauhusishi hivi vipengee viwili vilivyotajwa

Utamaduni ni kitu kinachoendelea na kilicho na sifa ya **Unyumbuaji** au **Unyumbulishaji.** Kinachosisitizwa hapa ni kwamba kila utamaduni huimarika, huchangamano kutegemea mabadiliko yanayojiri. Kwa hivyo utamaduni hupokea mambo mapya na kudondosha baadhi ya mambo.Na yasipondoshwa hufanyiwa marekebisho ilk yakubaliane na mpito wa wakati.

Utamaduni ni **Kuathiri** na **kuathiriana.** Hakuna utamaduni menyu. Hii inatokana na tabia ya watu kuingiliana. Watu wanaweza kuingiliana katika mambo mbalimbali. Wanaweza kuingiliana kibiashara, kidino, kisiasa, kimichezo, na kindoa. Kila wakati makundi ya watu yanapoingiliana hukutanisha tamaduni mbalimbali. Tamaduni hizi

zinapokutana, huathiriana. Inaweza kuwa kilugha, kitabia, kiimani, kimavazi, kikazi. Kwa hivyo tunaweza tukadai ya kwamba kila utamaduni una sifa za **umahuluti.**

Kwa sababu ya kuathiriana kwa tamaduni, kila utamaduni uliothiriwa huwa na elementi za **mionoulimwengu mbalimbali.** Hii ni kumaanisha ya kwamba kila wakati tamaduni mbalimbali zinapokutana mionoulimwengu ya watu hao huathirika. Falsafa yao ya maisha hupokea, hudondosha na kwekebisha mawazo yake. Mathalani, tulivyokwisha eleza katika sura zilizotangulia. Mwonoulimwengu wa waswahili husisha mionoulimwengu mingine- yaani mionoulimwengu ya makabila jirani kwa mfano wamijikenda, wapokomo, Wagalla na hali kadhalika mwonoulimwengu wa kiarabu. Vilevile sasa kuna athari za Kireno, Kiingereza na hata kihindi.

Utamaduni huwa ni dhima ya **utambulisho.** Lengo la utamaduni wowote ule huwa ni kuwatambulisha watu fulani miongoni mwa watu wengine. Hii ndiyo sababu utamaduni hung'ang'ania **upekee** wa aina fulani utakaovipa utambulisho huu. Ni kutokana na upekee huu tunaweza kuzungumzia kuhusu utamaduni wa waswahili, utamaduni wa Wachina, utamaduni wa Wanyamwezi, utamaduni wa Wareno.

Utamaduni **hukua;** kila utamaduni hukiuka mipaka ya wakati. Tayari tumesema kwamba utamaduni hupokea, hudondosha na hujirekebisha ili kuafikiana na kila kipindi cha wakati. Hali hii nayo vilelevile huathiri mwonoulimwengu wa jamii fulani. Kutokana na maelezo haya, hatuwezi kutoa kauli ya jumla kuhusu mwonoulimwengu wa watu fulani bila kutaja kipindi. Kwa mfano tunaweza kuzungumzia kuhusu mwonoulimwengu wa waswahili kabla ya Majilio ya ukoloni; au mwonoulimwengu wa Waswahili wakati wa

ukoloni, au mwonoulimwengu wa Waswahili wakati wa Majilio ya Waarabu au mwonoulimwengu wa Waswahili. Miongo miwili iliyopita.

Isitoshe ni muhimu kuweka bayana ni kundi lipi la Waswahili au sehemu ipi Uswahilini unayozungumzia. Tunasema hivi kwa sababu, dhana ya Waswahili na Uswahili imezua mijadala mingi sana kiasi cha baadhi ya wataalamu kudai kwamba waswahili walikuwa ni machotara ambao hawakuwa na utamaduni wao asilia. Knappert (1979: XI)

Kila utamaduni una **uamilifu mahsusi kupitia kwa asasi zake mbalimbali** Asasi za utamaduni hutoa mwongozo kuhusu namna watu wanavyoishi, mpangilio wa mambo mbalimbali katika jamii. Aidha uaminifu au dhima ya asasi hizo huelezewa. Baadhi ya asasi hizi ni kama vile; asasi ya ndoa, asasi ya tohara, asasi ya harusi, asasi ya utawala, asasi ya kielimu, asasi ya malezi. Tasnifu hii imeziangaza baadhi ya asasi hizo katika kazi ya Carl Velten: **Desturi za Waswahili.** Na Waswahili waliorejelewa ni wale wa Mrima. Na kama tulivyoona, asasi hizi ndizo zinazotuelezea kuhusu mwonoulimwengu wa watu hawa.

Utamaduni ni tukio la **Kibunifu na kiujumi,** kila utamaduni huwakilisha mfumo wa mawazo na maarifa ya jammi fulani. Mawazo na maarifa haya hutokana na ubunifu wa akili za watu hawa. Hakuna jamii isiyobuni. Maisha ni mkururo wa matukio mengi ya kibunifu. Ubunifu wa mawazo haufanywi tu kiholela mbali hufanywa kwa njia ya ufundi.Ufundi wa kubuni hulenga kuwacha athari ya kudumu miongoni mwa wapokezi wa mawazo au maarifa yanayobuniwa.

Utamaduni **husambazwa na kuhifadhiwa.** Kila utamaduni husambazwa na kuhifadhiwa iii usipotee. Unasambazwa iii kusisitiza upekee wake miongoni mwa tamaduni zingine. Na utamaduni huo huhifadhiwa iii usipotee au usife. Kupotea na kufa kwa utamaduni ni kufa kwa jamii nzima. Kwa mfano katika Kiswahili methali **"Mwacha mila ni mtumwa"** hutilia maanani umuhimu wa Mswahili kuhifadhi utamaduni wake utamaduni uanaweza kuhifadhiwa na kusambazwa kwa njia mbalimbali. Kama vile kupitia kwa nyimbo, hadithi, maandishi, sanaa mbalimbali-uchoraji, utarizi, vinyago, ususi, uhunzi, ushairi, vyombo vya habari, kufundishwa shuleni, kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya kuhifadhi, majina ya watu, vitu na mahali, kazi mbalimbali za watu hao, mavazi yao, sherehe mbalimbali.

Kazi hii imeshughulikia uhifadhi wa utamaduni wa Waswahili. Jambo linalosisitizwa na Chiraghdin(1977) anaposema ya kwamba waswahili walikuwa na namna yao ya kuhifadhi na kusambaza utamaduni wake kupitia kwa sherehe na sasi mbalimbali, na fasihi. Mbali na njia tulizozitaja, siku hizi kila mwaka, sherehe za kitamaduni, za maulidi huandaliwa katika miji mbalimbali ya Uswahilini kama vile Mombasa na Lamu. Lengo likiwa kueneza utamaduni wa Kiswahili. Isitoshe njia za kisasa za mawasiliano kama vile redio, runinga, mtandao wa "Internet", zimetumiwa kusambaza utamaduni. Muziki, mashairi na maigizo hupata fursa ya kuifikia hadhira pana zaidi. Si hayo tu maonyesho na sherehe huandaliwa na katika hoteli na mikahawa mbalimbali mfano **Swahili Night,** miongoni mwa sherehe zingine za kitamaduni zinazoandaliwa na Hotel ya Carnivore jijini Nairobi kila mwaka. Sherehe hizi huandaa vitu mbalimbali vinavyoambatana na utamaduni wa Kiswahili-muziki wao, mavazi, chakula n.k vilevile na muhimu kutambua

kazi zilizofnywa na wataalanu mbalimbali waliofanya utafiti wakakusanya habari zinazohusiana na utamaduni. Miongoni mwa wataalamu hawa ni Sheikh Ahmed Nabhany, aliyefanya utafiti mkubwa na kuandika kazi nyingi zinazozungumzia utamaduni wa Kiswahili. Sheikh Nabhany ametoa hotuba na mahojiano katika sehemu mbalimbali ulimwengu vikiwemo vyuo vikuu vingi.

Utamaduni huhifadhi **mawazo yake makuu.** Licha ya kuathiriana kwa tamaduni na hata kupokea na kudondosha mawazo, mawazo makuu au sifa kuu za utamaduni huo huhifadhiwa na kuboreshwa zaidi. Mawazo na sifa hizi ndiyo huwa uti wa mgongo wa utamaduni huo, ndiyo huupa upekee na utambulisho

Kazi ya Carl Velten: **Desturi za Waswahili** iliyohaririwa na Lyndon Harries inatupa fursa ya kufahamu falsafa ya Waswahili, hasa Waswahhili wa Mrima.Kuna zingine za aina hiyo mfano: **Kurwa na Doto** iliyoandikwa Muhammad S. Farsy , Kazi za aina hii ni muhimu kwa sabatu zinatusaidia kuelewa waswahili ni nani au ni watu wa aina gani. Uhakiki wa kazi za aina hii huchangia pakubwa kuelewa falsafa ya Waswahili. Jambo ambalo tungependa kupendekeza hapa ni kwamba utafiti ufanyiwe makundi mengine ya Waswahili kwa mfano Wamvita, waamu, wapemba wapate ilk utamaduni wa Kiswahili uweze kueleweka zaidi.

## MAREJELEO


Abdulaziz M. H. (1979) *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry.* Nairobi: Kenyj Literature Bureau.

(1995) "Impact of Islam on the Development of Swahili Culture' katika Bakari, M & Yahya S. S. (wahariri): *Islam in Kenyt* Mew Publications

Achebe, C. ( 1988) *Hopes And Impediments.* Nairobi: Heinemann Educationa Books Ltd.

Ani, M. ( 1996) 'The African Asili' Katika Ladner, J. A. na Gbadegesii (Wahariri) *Ethics, Higher Education And Socia Responsibility.* Washington: Howard University Press

Chiraghdin, S. na Mnyampala M. (1977) *Historiaya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University Press.

Diop, C. ( 1974) *The African Origin of Civilization Myth or Reality* Chicago Lawrence Hill & Co Ltd.

Farsy, M.S. (1960) *Kurwa na Doto.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Finnegan, R. (1970) *Oral Literature in Africa.* Nairobi: Oxford University Press

Harries, L. (1964) *Swahili Prose Texts.* London: Oxford University Press.

Irele, A *( 1981)* *The African Experience In Literature And Ideology.* Indiana: Indiana University Press

Kalu, O. U. (1991) "Precarious Vision: The African's Perception of His world" katika. Uka, E. M., Lang, P. (Wahariri) *The Readings in African Traditional Religions,*-European Academic Publications: Bern

Knappert, J. (1979) *Myths And Legends of the Swahili.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Leinhardt, P (1968) *The Medicine Man Swifa ya Nguvumali*_Oxford University Press; London

Lewis, J. (2002) *Cultural Studies.* London: Sage Publications.

*(1991)* *Culture Is Rutcm.* Nariobi: Longman Ltd.

Liyong, T. L. (1972) *Popular Culture Of East Africa.* Longman: Nairobi

Lyndon Harries (1964) *Swahili Prose Texts, OUP,* London

Maru, K.E. (1993) 'Nafasi Ya Nadharia Katika Uchambuzi Wa Fasihi Simulizi' Katika Gibbe A. G. (Mhariri) *The Spectator*, No. 1 Dar es Salaam: Education Service Centre Ltd.

Masolo, D A. (1994) *African Philosophy in Search of Identity.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mazrui, A. A. na Mazrui, A. M. (1995) *Swahili State and Society.* Nairobi: East African Educational Publishers

Mbiti, J.S (1966) *Akamba Stories.* Nairobi: Oxford University Press

(1969) *African Religions and Philosophy.* Nairobi: East African Educational Publishers.

McGee, J.R. na Warms, R. L. (2000) *Anthropological Theory An Introductory History.* California; Mayfield Publishing Company Toleo La Pili

Nangoli, Chief Musamaali (1987) *No More lies About Africa,*_2nd Edition, AH. Publishers,U.S.A

Njogu, K na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji ya Fasihi - Nadharia Na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Obiechina, E. N. (1990) *Language And Theme.* Washington: Howard University Press.

OhlyR (1981) *Aggressive Prose:* Dar es Salaam: TUKI

Okombo, O na Nandwa, J ( 1992) *Reflections on Theories and Methods in Oral Literature.* Nairobi: KOLA.

Okpekho, I. ( 1983) *Myth in Africa.* Cambridge: Cambridge University Press

Overholt, T. W. na Callicott, J. B. (2002) On The Ojibwa Worldview Katika Christensen, K.R. (Mhariri) *Philosophy and Choice.* California: Mayfield Publishers.

P'Bitek, O. ( 1989) *Song Of Lawino And Song of Ocol.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

PrinsA. J. H. (1967) *The Swahili Speaking Peoples of Zanzibar and The East African Coast,* London: International African Institute

Pritchard; E.E.E (1956) *Nuer Religion.*.Oxford University Press; Oxford

Ramose, M B. (2002) 'The Ethics Of Ubuntu' Katika Coetzee, P. H Na Roux, P. J. (Wahariri) *Philosophy From Africa*, Toleo La Pili Cape Town; Oxford University Press.

(2002) 'The Philosophy Of Ubuntu And Ubuntu As A Philosophy' Katika Coetzee, P H. Na Roux, P. J. (Wahariri) *Philosophy From Africa*, Toleo La Pili. Cape Town: Oxford University Press.

S. Rollins (1983) *A History ofSwahili Prose, E. J. Brill;Leiden*

Sartre, J. ( 1963) *The Wretched of the Earth.* Harmondsworth: Penguin Books Ltd.

Shariff, I. N ( 1988) *Tungo Zetu.* Treton: The Red Sea Press, Inc.

Soyinka W. (1976) *Myth, Literature And The African World.* Cambridge: Cambridge University Press.

(2002) 'Negritude And The Gods Of Equity' Katika Coetzee, P. H. Na Roux, P. J. (Wahariri) *Philosophy From Africa,* Toleo La Pili. Cape Town: Oxford University Press.

Vansina, J. (1985) *Oral Tradition As History*, Nairobi: East African Educationa Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi Ya Fasihi - Istilahi Na Nadharia.* Nairobi: Focu: Publications Ltd.

(2002) *Uhakiki Wa Fasihi - Misingi Na Vipengele Vyake.* Nairobi Phoenix Publishers Ltd.

*XSgSS&S^*

p 1T, M^0""